# MCHANGO WA VIJANA KULETA MABADILIKO CHANYA KATIKA TAMTHILIA TEULE ZA KISWAHILI

**NA**

**KIONGERA KIARIE J.**

**C50/64120/2010**

**Kazi Hii Imetolewa Kutosheleza Baadhi Ya Mahitaji Ya Shahada Ya Uzamili: Chuo Kikuu Cha Nairobi.**

**© JUNI 2012**

University of NAIROBI Library

0389166 0

## UNGAMO

Hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote kile

22/10/2012 ……………

Tarehe

Kiongera Kiarie J.

Mtahiniwa

Kazi hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

24/10/2012 ……………

Tarehe

Dkt. Mwenda Mbatiah

Msimamizi

28/10/2012 ……………

Tarehe

Dkt. Swaleh Amir.

Msimamizi

## SHUKRANI

Utafiti huu umekamilika kwa mchango na juhudi za watu wengi. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema, uzima wa mwili na akili timamu.

Shukrani za dhati nazitoa kwa wasimamizi wangu Dkt. Mwenda Mbatiah na Dkt. Swaleh Amiri kwa ushauri wao na uvumilivu mlionionyesha wakati wa kuandika kazi hii. Mola awabariki daima.

Shukrani za kipekee ziwaendee wahadhiri wangu wa Idara ya Isimu na Lugha wafuatao: Prof. Abdulaziz, Prof. Kithaka wa Mberia, Prof. Habwe, Dkt. Zaja, Dkt. Olali, Dkt Mukhwana Dkt Buregeya na Bw. Mungania. Utafiti huu ni matunda ya kazi yenu.

Shukrani za moyo zimwendee wangu kipenzi Bi. Leah wa Kiarie kwa mapenzi, uvumilivu, himizo na msaada alionipa kila mara nilipodidimia na kutamauka. *Mwathani Akurathime*. Kwa wanangu wapendwa Diana Gathoni, Kelvin Kiongera, na Joy Njeri- *Joseph* nasema asanteni kwa kunivumilia na kunihimiza tuliposoma pamoja. Kwa ndugu Dominiki nasema *thenkyu*.

Shukrani za kindugu kwa wasomi wenzangu darasani, Jacklyne Muthuri, Zipporah Rori, Pauline Kimani, Ferinda Kiende, Beatrice Mwandarani, Evaleyn Were na ndugu Amolo Najua tulikwama na kukwamuana mara si chache, mola awajaalie mnapopanda ngazi ya maisha.

Marafiki wangu wengi walinifaa kwa ushauri, Ndugu Omwaka, Ndugu Kanuri, Mbugua J., Dkt. Muhochi Sankai, Dkt. Wendo Nabea, Kariuki wa Ngugi, Wanjohi, Sammy Kiapo, Hon. Gaichuhie, Bw. Kamungu, Kibe, Kahuthu wa Muchemi, Ticha Isaac na wote walionipa moyo nilipokuwa nikisoma, Mungu awape kila mkihitajicho na kukitamani maishani mwenu.

## TABARUKU

Kwa marehemu wazazi wangu Kiongera wa Njoroge na Njeri wa Thuita. Nyinyi mlinileta duniani na kuniacha mapema. Mlitamani nisome. Kweli sasa nimeanza, ndiyo hii kazi ya digirii ya pili. Niko tayari kufuatilia ya tatu, Nawapungia mkono.

Kwa familia yangu, nawaenzi na nawapenda.

Kwa vijana nchini Kenya, kuweni chachu za maendeleo na mabadiliko nchini na nje ya nchi.

## YALIYOMO

Ungamo ii

Shukrani iii

Tabaruku iv

Yaliyomo v

Muhtasari viii

**SURA YA KWANZA**

1.0 Utangulizi 1

1.1 Tatizo la utafiti 5

1.2 Madhumuni ya utafiti 6

1.3 Nadharia tete 6

1.4 Sababu za kuchagua mada 7

1.5 Upeo na mipaka 9

1.6 Msingi wa nadharia 10

1.7 Yaliyoandikwa juu ya mada 15

1.8 Mbinu za utafiti 19

1.9 Hitimisho 20

**SURA YA PILI**

**VIJANA NA MAOVU WANAYOKABILIANA NAYO ILI KULETA MABADILIKO**

2.0 Utangulizi 21

2.1.1 Dhana ya vijana 22

**2.2 Maovu ya kisiasa** 25

2.2.1 Udikteta 26

2.2.1.1 Mkakati wa kuwatumia askari makatili 32

2.2.1.2 Mkakati wa kuwatumia ya makachero 34

2.2.1.3 Mkakati wa kuwatumia washauri makatili 35

2.2.1.4 Matumizi ya gereza na vitisho 37

2.2.2 Maamuzi mabaya 45

2.2.3 Kutozingatia Maadili 49

2.3 **Maovu ya Kiuchumi**

2.3.0 Utangulizi 54

2.3.1 Ufisadi 55

2.3.2 Ubadhirifu 61

3.4 Ulanguzi 62

2.4 **Maovu ya Kijamii**

2.4.0 Utangulizi 62

2.4.1 Chuki na vita vya kikabila 63

2.4.2 Unafiki na uongo 65

2.4.3 Dhuluma 66

2.4.4 Usaliti 70

2.4.5 Ukaragosi 71

## SURA YA TATU

## MAFANIKIO NA CHANGAMOTO ZINAZOWAKABILI VIJANA KATIKA HARAKATI ZAO ZA KULETA MABADILIKO


**3. Mafanikio**

3.0 Utangulizi 73

3.1.1 Kuwaondoa madikteta uongozini 73

3.1.2 Kubadili mawazo 76

3.1.3 Kuwatafuta viongozi wapya 77

3.1.4 Kufichua kashfa za ufisadi 78

3.1.5 Kutenda haki bila kupendelea 79

**3.2 Changamoto**

3.2.0 Utangulizi 80

3.2.1 Mitazamo hasi kuhusu vijana 80

3.2.2 Ushawisi wa viongozi walio madarakani 81

3.2.3 Vijana kutochukua tahadhari 83

3.2 4 Ukosefu wa mipango ya siku za baadaye 84


## SURA YA NNE


**HITIMISHO**

4.0 Utangulizi 86

4.1 Muhtasari wa utafiti huu 86

4.2 Matokeo ya utafiti 89

4.3 Mapendekezo 90

**MAREJELEO** 91

# MUHTASARI

Kazi hii inahusu juhudi za vijana kama mawakala wa mabadiliko chanya katika tamthilia nne za Kiswahili. Tamthilia hizi ni *Kifo Kisimani* na *Maua Kwenye Jua la Asubuhi* zilizoandikwa na Kithaka wa Mberia . *Pango* na *Seserumbe,* zilizoandikwa na K.W. Wamitila.

Tumeongozwa na nadharia ya Ki-Foucault iliyoasisiwa na Micheal Foucault. Huyu ni mwananadharia wa Kifaransa aliyeishi baina ya mwaka wa 1926 hadi 1984. Tunaangazia mtazamo wake kuhusu mahusiano ya mamlaka na upinzani unaozuka pale panapokiukwa maadili ya mahusiano yenyewe. Upinzani tunaouchanganua ni ule unaoongozwa na wahusika vijana katika tamthilia nne tulizoziteua.

Katika sura ya kwanza, tumechunguza maswala ya kimsingi yanayodhamiria kujenga msingi wa utafiti wetu kama vile: Sababu za kushughulikia mada, tatizo la utafiti, yaliyoandikwa kuhusu vijana, upeo na mipaka ya utafiti. Tumeongozwa na nadharia tete zifuatazo: kwamba vijana wamefanikiwa kuyaleta mabadiliko na kwamba wanakabiliwa na changamoto mbalimbali katika jitihada zao.

Katika sura ya pili tumeijadili dhana ya vijana na kuyachunguza maovu ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Hapo tumewaonyesha vijana wakikabiliana na maovu hayo ili kuleta mabadiliko chanya.

Katika sura ya tatu tumechunguza mafanikio waliyoyapata vijana katika kuzibadilisha jamii zao. Pia tumechunguza changamoto zinazowakabili katika harakati zao za kuleta mabadiliko chanya.

Katika sura ya nne tumetoa muhtasari wa utafiti mzima na mapendekezo ya tafiti zaidi zinazoweza kufanywa kuhusiana na mada yetu.

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Utafiti huu umejihusisha na swala la mahusiano ya mamlaka na mchango wa vijana katika kuyatatua matatizo yanayozikabili jamii kwa mujibu wa tamthilia nne za Kiswahili nchini Kenya. Sababu kubwa za kuishughulukia mada hii ni kuwa, maswala kuhusu mahusiano ya mamlaka na jinsi vijana wanavyochangia kuleta mabadiliko chanya yameonekana kupembezwa katika tafiti za kifasihi.

Kuna utata mkubwa kuhusu tafsiri ya kijana ni nani. Katika utafiti huu, tunazingatia kijana kuwa mwanadamu wa kiume au kike aliye kati ya umri wa miaka 15 na 35. Kipindi hiki cha maisha hudhihirika kuwa cha mpito, ambapo kijana huwa akibadilika toka maisha ya utotoni hadi utu uzima. Data ya kutetea uamuzi huu itatolewa katika sehemu inayoifasili dhana ya vijana.

Swala la mabadiliko pia huwa tata. Hii ni kwa sababu mabadiliko yanaweza kuwa chanya au hasi. Mabadiliko chanya hufaidi jamii ilhali yale hasi huzorotesha hali za watu. Utata hutokea kuhusu tofauti baina ya faida na hasara kwa sababu, jamii mbalimbali huwa na mizani na mitazamo tofauti ya kukadiria faida au hasara. Kuna jamii ambazo hupuuza mabadiliko yoyote yasiyofuata maadili yake. Kwa uzingatifu wa utata huu, utafiti wetu unazingatia mabadiliko chanya yenye kufuata maadili ya jamii tunazokumbana nazo katika tamthilia nne tulizoziteua.

Mabadiliko haya, yatakuwa ni kutokana na uvunjaji wa maadili katika mahusiano ya mamlaka yanayosababisha mifumo dhulumati, utumizi mbaya wa mali ya umma,vita vya kikabila, ukatili na maovu mengineyo. Kwa jumla tunazihakiki tamthilia nne zilizo na maudhui ya ukiukaji wa maadili ya mamlaka yanayoishia kwenye uongozi mbaya.

Utafiti huu unadhamiria kuonyesha kuwa wahusika vijana ni mawakala wafanisi wa mabadiliko. Ushahidi wa dai hili umetolewa katika tamthilia nne za Kiswahili zilizochapishwa katika mwongo wa kwanza wa karne ya ishirini na moja. Tamthilia hizi ni: *Kifo Kisimani,* (2001), *Pango,*(2003), *Maua Kwenye Jua la Asubuhi,* (2004) na *Seserumbe,* (2009). Katika kazi hizi za kisanii, vijana wameonyeshwa kama wanajamii waliojizatiti kuwa mstari wa mbele katika kuleta mabadiliko chanya yenye kuwafaidi wanajamii wote walionyimwa haki, kunyanyaswa na kudhulumiwa kwa njia mbalimbali.

Nchini Kenya, kuna kauli maarufu sana kuwa '*vijana ni viongozi wa kesho*'. Hii ni kauli ambayo hutolewa mara kwa mara na viongozi katika nyanja nyingi ili kuwapa vijana moyo na hapohapo, kuchelewesha kutambuliwa kwao kama wanajamii wenye uwezo wa kuongoza kwa wakati uliopo. Kipragmatiki, kauli yenyewe ni utambuzi wa viongozi kwamba kuna wakati ambapo vijana watachukua hatamu za uongozi. Swali kuu linakuwa, wakati huu utafika lini na zipi ndizo zitakazokuwa dalili zake? Utafiti huu kwa hivyo, utakuwa ni tathmini ya dalili zinazojitokeza katika tungo za kifasihi.

Katika tamthilia tunazozihakiki vijana wanadhihirisha kuwa wanafaa kutambuliwa kama kiungo muhimu na washika dau katika jamii. Wamejitokeza kama mawakala wenye uwezo wa kuleta mabadiliko. Wamefanya hivi kwa kuwazindua wanajamii na kuwaonyesha ukweli

wenye kuudhihirisha uozo wa viongozi waliopewa nyadhifa za kufanya maamuzi kwenye asasi mbalimbali.

Tunaangalia jinsi jamii katika tamthilia hizi nne zinavyoendesha mahusiano ya kimamlaka. Kwa upande mmoja, tunawaangazia viongozi waliopo madarakani, ambao wameendelea kung'ang'ania kuwa vijana ni wazua fujo, wasiojua chochote, wachochezi na wasaliti wa maadili ya kijamii yenye uzingatifu wa kunyenyekea na kuwatii viongozi. Kusudi lao kuu likiwa ni kuwahimiza wanajamii kuwapuuza vijana ili wasipewe mamlaka katika jamii.

Viongozi waliopewa mamlaka na raia, wanajitahidi kuzishikilia nyadhifa mbalimbali katika mifumo dhulumati waliyoizua. Wanayafanya hayo kwa kueneza uongo, fitina na vitisho kwa madai kuwa vijana hawa wataleta fujo, hawapendi maendeleo na hawana ujuzi wa kuifahamisha jamii lolote. Kulingana na utafiti wetu, njia hizi za viongozi, ndiyo mikakati ya viongozi kujitahidi kudumu mamlakani ambayo anaizungumzia Foucault (2000).

Ni kwa sababu hii ndipo tumeipigia darubini jamii kwa kuitazama kwa pande mbili. Upande mmoja tunazichunguza asasi ambazo zina uhafidhina wenye kuwadhulumu wanajamii. Kwa upande wa pili, tunaangalia jinsi vijana wanavyowazindua wanajamii katika kuyatambua maovu na hatimaye, kuleta mabadiliko yenye kuwapa wanajamii matumaini. Wanajamii hatimaye wanajinasua kutoka kwenye mifumo hiyo dhulumati, gandamizi na nyanyasaji.

Kazi hii pia inadhamiria kuonyesha kuwa, kuna makundi mbalimbali yanayoshindania nguvu za kiutawala na kimaamuzi kuhusu maswala muhimu katika jamii. Kwanza, kuna kundi la watu kwenye nyadhifa za kiuongozi katika viwango tofauti kama vile kitaifa, kieneo na kiwizara ambao wana mamlaka na nguvu za kisiasa, kisheria, kiuchumi na kitamaduni. Kwa

sababu hii, wanatumia mamlaka waliyopewa kujifaidi wenyewe bila kuwajali wanajamii. Kundi hili pia linajumuisha wafuasi sugu, vikaragosi na vibaraka wanaowafuata viongozi hao kijanjajanja ili kujifaidi kibinafsi.

Kundi la pili tunalolimulikia kwa kiwango kikubwa, ni lile la wahusika vijana. Hawa ni wahusika ambao wana nishati, hisia na mitazamo mipya kuhusu maswala ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Mitazamo hii mipya inawapa uwezo wa kuibuka na njia badalia za kutatua matatizo ya wanajamii wote kwa jumla.

Hapa vijana wameonyeshwa namna wanavyokabiliana na matatizo dhulumati katika jamii. Wanaonyeshwa kama wanajamii walio tayari kukabiliana na viongozi wakatili, mafisadi, na wenye fikra za kihafidhina zinazounga mkono viongozi walewale ili waendelee kubakia kwenye nyadhifa za uongozi hata pale wasipowajibika katika utekelezaji wa majukumu waliyopewa.

Vijana wameonyeshwa kama watu wenye uwezo wa kuyagundua maovu, kuwazindua wanajamii wengine, kuwahimiza, kuwapa shime wenzao ili waungane na kuyaondoa mamlaka dhulumati na yenye kukandamiza haki za watu wengi. Tumeonyesha changamoto na vikwazo vinavyowakabili vijana katika jitihada zao za kuleta mabadiliko. Changamoto hizi ni zile zinazosababishwa na mikakati ya viongozi wanaonuia kudumaza jitihada zao. Pia kuna changamoto zinazosababishwa na upungufu wao wenyewe kutokana na ukosefu wa tajiriba au mitazamo hasi ya kutowaamini na kuwabagua vijana katika nyadhifa za kimaamuzi.

Kwa hivyo, swala la kimsingi la utafiti huu ni kuonyesha vipengele muhimu vya mahusiano ya mamlaka na namna vijana wamejitokeza kama mawakala wa mabadiliko kutokana na kutozingatiwa maadili yanayotawala mahusiano hayo.

## 1.1 TATIZO LA UTAFITI

Vijana kama mawakala waliofanikiwa kuleta mabadiliko yenye kuwafaidi wanajamii kisiasa, kiuchumi na kijamii katika tamthilia za Kiswahili ni swala linalostahili kufanyiwa utafiti. Hili ni swala muhimu kwa vile halijashughulikiwa kwa mtazamo tunaouchukuwa katika utafiti huu.

Hili ni tatizo linaloonyesha mchango wa vijana katika kuleta mabadiliko chanya katika jamii kama wanavyosawiriwa katika tamthilia teule zilizochapishwa mwanzoni mwa karne ya ishirini na moja. Kwa maneno mengine, tunachunguza mtagusano wa vijana na walio mamlakani ambao, aghalabu ni wazee wasiotaka kuyaachilia; kwa upande mwingine kuna vijana waliotengwa kutoka kitovu cha madaraka na ambao wanaipinga hali hii.

Hili ni suala zito ambalo linahusu utambuzi wa vijana kwamba, wao ni washika dau muhimu katika jamii zao na wako tayari kupigana na nguvu zozote zinazojaribu kuwapembeza. Kwa kuwa vijana ndio walio wengi katika jamii, mwamko wao ni dalili muhimu ya majilio ya jamii mpya. Haya ni maudhui yanayoangaziwa na tamthilia zilizochapishwa hivi karibuni kama juhudi za waandishi kuonyesha jinsi jamii inavyobadilika. Ni maudhui ambayo hayajafanyiwa utafiti wa kina kama tunaoufanya kwa kuzihakiki tamthilia nne zinazowakilisha mwelekeo huu.

Maswali tunayojaribu kujibu katika utafiti huu ni kwanza, je vijana wamechangia mabadiliko yapi na kwa kiasi gani katika jamii? Pili, je wamefaulu kuleta mabadiliko? Tatu ni je wanakabiliana na changamoto zipi katika jitihada zao?

Kwa kifupi, swala letu la utafiti ni kuwa: Vijana wamechangia na kujitokeza kama mawakala waliofaulu kuleta mabadiliko chanya katika jamii kulingana na tamthilia nne zilizochapishwa katika mwongo wa kwanza wa karne ya ishirini na moja.

## 1.2 MADHUMUNI YA UTAFITI

1. Kutambua maovu ya kisiasa, kiuchumi na kijamii yanayozua migogoro na yanayohitaji kubadilishwa kwa ushahidi ulioko katika tamthilia nne tulizoziteua.
2. Kuthibitisha mchango wa vijana katika juhudi za kuleta mabadiliko chanya katika jamii kama inavyojitokeza katika tamthilia nne za Kiswahili zilizochapishwa katika mwongo wa kwanza wa karne ya ishirini na moja.
3. Kutathmini ufanisi na changamoto zinazowakabili vijana katika harakati zao za kuleta mabadiliko chanya katika jamii zao.

## 1.3 NADHARIA TETE

Utafiti huu umeongozwa na nadharia tete zifuatazo:

- Kuna maovu ya kisiasa, kiuchumi na kijamii yanayozua migogoro na yanayohitaji kubadilishwa katika tamthilia nne tulizoziteua.
- Vijana ni mawakala wafanisi katika juhudi za kuleta mabadiliko chanya katika jamii zenye maovu ya kiuchumi, kisiasa na kijamii kutokana na ushahidi uliopo kwenye tamthilia nne tulizoteua.
- Vijana hukabiliwa na changamoto mbalimbali katika harakati zao za kuleta mabadiliko chanya katika jamii.

## 1.4 SABABU ZA KUICHAGUA MADA

Katika tamthilia tunazozihakiki vijana wanajitokeza kama nguvu mpya inayofaa kutambuliwa katika mahusiano ya mamlaka kwa namna wanavyochangia kuleta mabadiliko katika jamii. Haya yamejitokeza wazi katika tamthilia nne tulizoziteua.

Hapajakuwa na uhakiki wa tamthilia kwa mtazamo tunaouzingatia wa kuwa, vijana ni mawakala wa mabadiliko chanya. Tahakiki za hapo awali zimewasawiri vijana kama watu wachanga waliokengeuka, wanaojiingiza katika mivutano anuwai kutokana na tofauti za vizazi, waliokosa maadili na wanaojishughulisha na maswala ya kibinafsi kama vile ya kimapenzi na utovu wa mbeko na nidhamu.

Katika tamthilia tunazozihakiki, vijana wamefaulu kwa kiwango kikubwa kuzikomboa jamii zao. Wameweza kuleta hali nafuu dhidi ya mifumo dhulumati, yenye kutumia mamlaka vibaya, fisadi na yenye kuzua migogoro ya kijamii iletayo vita na maafa.

Kuna sababu kadha zilizotufanya kuziteua tamthilia hizi. Kwanza zinaafiki mada yetu vizuri. Hii ni kwa sababu maudhui ya mabadiliko yamejitokeza na kukuzwa kisanii na kwa kuridhisha.

Pili, wahusika vijana wamajumuishwa kuchangia katika maudhui ya mabadiliko, ambayo ndiyo tunayolenga kuyahakiki. Maudhui hayo yamekuzwa kikamilifu, hivyo kuweza kufanikisha utafiti wetu.

Tatu, katika tamthilia zote nne, motifu ya vijana kama mawakala wa mabadiliko chanya inajitokeza. Wahusika vijana wametumika kuyashughulikia matatizo mbalimbali yaliyoko kwenye jamii zao. Matatizo hayo ni ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Vilevile tamthilia zenyewe ni mpya na hazijafanyiwa uhakiki kwa mtazamo wa kuwachanganua vijana kama mawakala wafanisi wa kuleta mabadiliko chanya katika jamii zao.

Kiuhalisia, mada yetu ni muhimu kwa kuzingatia kuwa, taifa la Kenya limeanza kuyatilia maswala ya vijana umuhimu. Katiba mpya ya Kenya (2010), sehemu ya 3, ibara ya 55 kipengele cha kwanza hadi tano, haki za vijana zimetambuliwa rasmi. Vilevile vijana sasa watakuwa na wawakilishi wao katika bunge na sehemu mbalimbali za kitaifa. Maswala ya vijana ni muhimu pia kwa kuzingatia kuwa idadi yao, kulingana na makadirio ya idadi ya watu ya mwaka wa 2009 ni kubwa. Kulingana na Njonjo, (2010) idadi ya vijana wa kati ya miaka 15 hadi 35 ni milioni 13, ambayo ni asilimia 56 ya jumla ya watu nchini Kenya.

Hii inamaanisha kuwa maswala ya vijana hayawezi kupuuzwa. Hii ndiyo sababu tunazihakiki tamthilia hizi ili kuona namna wasanii wanavyowahusiha vijana katika jamii wanazozisawiri. Hapa mawazo haya yanatiliwa uzito na kauli ya Aristotle katika Dorsch(1965), kuwa:

> … fasihi ni umitilishaji wa vitendo vya mwanadamu.
> Kwa umithlishaji anamaanisha uwakilishaji katika
> misingi yake. [tafsiri yetu]

Hii inaashiria uwezekano mkubwa kuwa hali kama ilivyo kwenye fasihi inaweza kutokea katika maisha halisi.

Wamitila ( 2008:338-339) akizungumzia fasihi ya vijana anasema kuwa:

> … pamekuwepo na pengo kubwa katika ushughulikiwaji
> wa fasihi hiyo kwa vile kuna maandishi machache ya

kinadharia kufidia pengo lenyewe.

Ijapokuwa kazi tulizoziteua si fasihi ya vijana kamili, zinazingatia vijana kama wahusika wakuu ambacho ni mojawapo ya vipengele vinavyoitambulisha fasihi ya vijana. Utafiti wetu unawatumia wahusika hao kama kigezo cha kukadiria mabadiliko na kwa hivyo utafiti huu unachangia kuziba pengo analolizungumzia mtaalam huyu.

## 1.5 UPEO NA MIPAKA

Utafiti huu umehusisha kusoma na kuchanganua vipengele vya dhamira, maudhui na wahusika katika tamthilia. Tumezihakiki tamthilia zifuatazo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. *Kifo Kisimani* | Wa Mberia K. | (2001) |
| 2. *Pango* | Wamitila K.W | (2003) |
| 3. *Maua Kwenye Jua la Asubuhi* | Wa Mberia K. | (2004) |
| 4. *Seserumbe* | Wamitila K.W. | (2009) |

Tumezichagua tamthilia hizi kwa sababu miongoni mwa tamthilia nyingine tilizozisoma, hasa zilizoandikwa katika mwongo wa kwanza wa karne ya ishirini na moja nchini Kenya na kuyashughulikia maswala ya mabadiliko chanya yanayochangiwa na vijana, tuliziona hizi nne kama zinazowakilisha mada yetu kwa mtazamo bora zaidi. Miongoni mwa tamthilia zingine tulizozipitia ili kuziteua hizo nne ni kama vile; *Sumu ya Bafe, Natala, Mnara wa Sokomoko, Migogoro, Sudana, Janga la Werevu, Kijiba Cha Moyo* na *Chamchela* miongoni mwa zingine.

Tamthilia nne tulizoziteua zinazingatia maudhui ya mabadiliko katika jamii na kujumuisha wahusika vijana wanayoyashughulikia. Vigezo hivi viwili vya maudhui na wahusika ni

muhimu sana katika utafiti wetu, hasa tukizingatia kuwa, vimeshughulikiwa kwa njia mwafaka.

Tamthilia hizi ni mpya na hazijahakikiwa kwa mtazamo tuliouchukua. Zimeishughulikia mada yetu kwa kina na kuakisi hali zilizoko kwenye jamii kwa njia inayofaa.

## 1.6 MSINGI WA NADHARIA

Katika utafiti huu tumeongozwa na nadharia ya Ki-Foucault, haswa mtazamo wake kuhusu mahusiano ya mamlaka na upinzani. Nadharia ya Ki-Foucault inahusishwa na Micheal Foucault, mwananadharia wa Kifaransa aliyeishi kati ya mwaka wa 1926 na 1984.

Foucault anaonyesha uhusiano wa mamlaka kama hali changamano na kitu kinachobadilikabadilika. Watu huweza kuathiriana katika maingiliano yao na kudhihirisha kwamba kila mtu katika jamii huwa na mamlaka yake. Mamlaka haya husambaa kimtandao, nao watu binafsi huwa katika nafasi ya kuongozwa ama kuongoza kwa wakati uo huo. Hali hizi huwafanya watu kujitokeza kama walengwa na waenezaji wa mamlaka. (Dreyfus, 1982).

Tumeonyesha kuwa katika tamthilia tulizoziteua jamii mbalimbali hustawisha mahusiano ya mamlaka kwa kuwapa viongozi idhini ya kuwaongoza. Hii ni kwa kuzingatia mawazo ya Sercombe, (1997) anaposema kuwa:

> …kila mtu huwa na mamlaka na huyatoa kwa kiongozi
>
> kwa idhini yake mwenyewe ili awakilishwe,
>
> idhini hutolewa kwa imani kuwa kiongozi huyo
>
> atazingatia maadili ya mahusiano ya mamlaka.(tafsiri yetu)

Katika tamthilia nne tulizoziteua, kuna jamii zinazodhihirisha mahusiano ya mamlaka yanayokumbwa na upinzani kutokana na viongozi wasiozingatia maadili ya mahusiano yenyewe. Jamii tutakazozichunguza ni zile za Wanabutangi katika *Kifo Kisimani* wakiongozwa na Mtemi Bokono. Wachemwa katika *Pango* wakiongozwa na Ngwese. Wandiku na Watange wa Wilaya ya Loloma chini ya uelekezi wa Kabitho na Chebwe katika *Maua Kwenye Jua la Asubuhi* na wafanyakazi wa wizara ya Utandawazi,Uchukuzi na Teknohama chini ya waziri Seserumbe katika tamthilia ya *Seserumbe*.

Kulingana na Foucault (2000), maisha yasiyo ya kifashisti au kidikteta yanaweza kuafikiwa iwapo mambo kadha yanaweza kufanywa. Kulingana naye wanajamii wanaweza kushiriki katika vitendo huru na chanya vya kisiasa kwa kuzua mikakati yenye kuleta mabadiliko. Vitendo hivi vinafaa kuegemea kwenye mifumo yenye kuwaunganisha watu badala ya kuwatenganisha. Kwa njia hii, mapinduzi yanaweza kuafikiwa bila kutumia fujo wala misukasuko kwa vile watu watazingatia hali halisi na mahitaji katika jamii husika. Katika tamthilia tunazozihakiki, tunaona vile wanajamii wakiongozwa na vijana wanaungana ili kuleta mabadiliko kutokana na matatizo halisi yanayowakabili.

Tumewateua vijana kama kigezo cha kuchanganulia mabadiliko katika asasi mbalimbali kama inavyojitokeza katika tamthilia teule. Hii ni kwa kuzingatia kwamba, wahusika vijana katika tamthilia hizi wanajitokeza kama kundi muhimu la wanajamii wenye mawazo na maarifa yanayoweza kuleta mabadiliko chanya.

Foucault anatambua kuwa, kuna maadili yanayohusu mahusiano ya mamlaka. Maadili haya yanahusu jinsi mahusiano yenyewe yanafaa kuendeshwa. Baadhi ya maadili yanahusu uhalali wa viongozi, uadilifu wa washika dau, na haki za kila mwanajamii. Huwepo kuna kanuni za utofautishaji kuhusu mamlaka ambayo kila mmoja hupewa na sheria, uchumi, madaraka na vyeo katika mahusiano.

Katika tamthilia zote nne tunaona kuwa watu wamepewa nyadhifa, vyeo na majukumu mbalimbali. Kuna viongozi wakuu, mawaziri, washauri wa viongozi, makachero, askari na raia. Kuna pia wazazi ambao ni viongozi katika familia, wazee wa kikabila, viongozi wa wafanyakazi na vijana wenye ushawishi mkubwa.

Katika tamthilia tulizoziteua, tunachunguza kwa jinsi ambavyo viongozi kama Bokono, Ngwese, Seserumbe, Kabitho na Chebwe wanavyoyatumia mamlaka waliopewa na raia. Tumechunguza viwango vya uzingatiaji au utozingatiaji wa maadili katika mahusiano ya mamlaka na athari zake kwa raia waliowachagua.

Foucault anatambua kuwa katika mahusiano ya mamlaka huwa kuna mikakati ya wanaoongoza na wale wanoongozwa. Kwanza kuna viongozi wenye mamlaka makubwa na wawakilishi wa maslahi ya raia. Mikakati yao hulenga kufaulisha na kudumisha mifumo iliyopo ili wabakie madarakani. Hii huwafanya wahakikishe kuwa raia wametii na kufuata sheria zilizowekwa kwa kutumia vyombo vya serikali. Upande wa pili hujumuisha raia waliotoa idhini ya mamlaka yao kwa viongozi ili wawawakilishe na kufanya maamuzi kwa niaba yao. Hawa huzua mikakati ya upinzani pale wanapoona kuwa viongozi wamekiuka maadili ya mahusiano.

Katika tamthilia tulizoziteua tunaona jinsi viogozi wanavyojidumisha mamlakani kwa kutumia mikakati anuwai. Kwa kiwango kikubwa tamthilia tulizoziteua zinawasawiri viongozi kama watu wasiozingatia maadili. Wanatekeleza maovu yanayopelekea raia waliowapa mamlaka kuteseka. Vijana katika jamii hizi, wanapogundua ujanja na maovu ya viongozi wao, wanafanya jitihada za kubadilisha hali mbaya zilizopo. Kwa njia hii wanajitokeza kama mawakala wa mabadiliko ili kuwaondoa viongozi hao waovu madarakani.

Foucault (2000), anatambua kuwa kila mahusiano ya mamlaka huzua harakati za kuyapinga hasa panapozuka ukandamizaji. Tunakizingatia kipengele hiki cha nadharia ya Ki-Foucault

kuchanganua upinzani unaozuliwa na vijana katika tamthilia tulizoziteua. Kwa kiwango kikubwa, upinzani unazuka kutatokana na mifumo dhulumati na kandamizi, ufisadi, ukosefu wa utu, chuki na vita vya kikabila na maovu mengine ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Tumeuonyesha ufanisi waliouafikia vijana katika juhudi zao za kupigania haki za kibinadamu. Vijana wanajitokeza kama nguvu ya kutambulika katika kupigania haki hizo na tunachunguza ufanisi wanaoupata katika jitihada zao.

Katika tamthilia ya *Kifo kisimani,* vijana wakiongozwa na Mwelusi, wanatoa upinzani baada ya kuzuka migogoro kutokana na marufuku iliyowekwa katika matumizi ya kisima cha maji. Utawala wa Bokono unamtia Mwelusi gerezani ili kuzima upinzani wenyewe. Nao raia wanazua mikakati ya kumsaidia kijana huyu kutoroka gerezani.

Katika tamthilia ya *Pango*, Ngwese analiongoza pango la Wachemwa kwa ubinafsi mkubwa, Yeye pamoja na raia wachache wanashirikiana na wakoloni katika kuipora hazina ya pango. Jambo hili linazua upinzani unaoongozwa na Katango ambaye anazielewa hila na njama za Ngwese. Mwishowe Katango anafaulu kumfumanisha Ngwese na wenzake wanapokuwa wakilihujumu pango.

Katika tamthilia ya *Maua Kwenye Jua la Asubuhi,* tunashuhudia mgogoro wa kikabila baina ya Wandiku na Watange. Kuna uchochezi mwingi baina ya makabila haya mawili unaoongozwa na Kabitho na Chebwe. Upinzani dhidi ya kushiriki katika vita vya kikabila unazuliwa na vijana wawili, Waito ambaye ni Mndiku na Nali ambaye ni Mtange. Vijana hawa wanawahimizi viongozi hao wa kikabila kutafuta njia badalia za kutatua migogoro yao badala ya vita.

Katika tamthilia ya *Seserumbe*, tunakumbana na waziri Seserumbe ambaye anaziendesha shughuli katika wizara kama milki yake binafsi. Upinzani unazuliwa na Kembo ambaye ni

kijana mhasibu katika wizara. Katika uchaguzi wa ubunge, Kembo anamshinda Seserumbe na hivyo anapokonywa uwaziri na hatimaye kushtakiwa.

Foucault pia anatambua kwamba, katika mahusiano ya mamlaka, huwa kuna kipengele muhimu cha mawazo na mielekeo ya ukweli. Wamitila (2002:171), akichambua nadharia ya Ki-Foucault anasema kuwa, kila awamu au kipindi huwa kinatawaliwa na mielekeo au mikabala maalum kuyahusu maarifa ambayo Foucault aliyaita *episteme*. Anatoa mfano wa matumizi ya gereza kuonyesha jinsi mamlaka rasmi katika jamii ya kisasa yanavyotegemea kwa kiasi kikubwa, udhibiti wa mkondo wa mawazo na maarifa ya watawaliwa na mamlaka hayo.

Katika tamthilia nne tunazozihakiki ni bayana kuwa, viongozi tunaokumbana nao wanajua kutumia sheria na semi kama mikakati ya kuzima upinzani dhidi ya mamlaka yao. Katika *Kifo Kisimani,* Bokono anahakikisha kuwa Mwelusi amechorwa kama mchochezi katika akili za Wanabutangi badala ya mpiganiaji wa haki za wanajamii wanaonyanyaswa. Sheria zilizopo Butangi zilimruhusu Mtemi kumhukumu 'mchochezi' kwa kumtia gerezani, kumtisha na kumtesa. Vilevile anatumia ushawishi wa kumpa Mwelusi mali ili atangaze hadharani kuwa, yeye ni mchochezi aliyebadilika na hivyo kuwaomba Wanabutangi msamaha. Kwake Bokono, jambo hili lingehalalisha mamlaka yake dhulumati.

Katika tamthilia ya *Seserumbe*, Waziri mwenyewe katika kampeni zake, anachora picha ya namna vijana wasivyokuwa na tajriba ya kuongoza. Hivyo anawahimiza wapiga kura wasimwamini Kembo hata kidogo kwa vile ni kijana. Vilevile anatumia ukosefu wa ajira kama sababu ya kuwatumia vijana vibaya katika kulangua mihadarati. Kinafiki Seserumbe anasingizia kwamba, alikuwa amewapa vijana ajira ya kuuza njugu na unga ambavyo ni vyakula vya kawaida huku Kembo akiueleza ukweli peupe.

Katika tamthilia ya *Pango,* Ngwese anamdhihaki Katango kwa kumuita kijana na mwanamke asiyeelewa chochote, anawashawishi wapiga kura wasimdhamini kwa kuwa alikuwa kijana na hakutoka katika nyumba ya viongozi. Jambo hili la kurithishana uongozi linaonekana kushamiri katika jamii tunazozichanganua. Viongozi waliopo wakiwa wanatawaliwa na kasumba ya kuwa, koo zao ni kuu na zinapaswa kutawala milele bila kujali iwapo wanapendwa au la.

Waito na Nali katika tamthilia ya *Maua Kwenye Jua la Asubuhi*, wanapojua kuhusu matayarisho ya vita ambayo yalikuwa yakifanywa na makabila yao, wanaamua kuwashawishi wafadhili wa vita kutoka pande zote mbili. Ukweli wanaotarajiwa kuufahamu kutoka kwa wazee wao ni kuwa, kila kabila lilifaa kujihami. Kinyume na imani ya wazee wao, vijana hawa wanazuka na ufahamu mpya kutokana na tajriba waliyokuwa nayo baada ya kuzuru maeneo yaliyokuwa yamekumbwa na vita vya kikabila. Maeneo hayo kama wanavyowafahamisha wazazi wao, yalikuwa yamezifuata njia hizo za kujikinga na kujihami kikabila. Vijana hawa wawili wanawatahadharisha wakuu wao kwamba, vita vya mishale vingalifuatwa na zana kali zaidi hadi kufikia kuuana kwa mabomu na mabazuka. Hatimaye, ukweli mpya wanaouibua unakuwa ni njia ya kumaliza vita na hivyo Waito na Nali ambao ni vijana wanajidhihirisha kama mawakala wafanisi wa kuleta mabadiliko chanya katika jamii yao.

## 1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

Uhinga na Mungai (Topan, 1975), wakihakiki tamthilia ya *Nakupenda Lakini* (1957) wanaonyesha kuwa tamthilia hii ilikusudiwa kuwaburudisha watazamaji, ambayo kweli ni kauli ya mwandishi katika utangulizi wa tamthilia yenyewe. Kulingana nao, maudhui yaliyomo yanahusu mapenzi baina ya vijana. Wanaona kuwa, vijana hawakuchangia kwa njia yoyote katika maswala yaliyowakabili wanajamii. Japokuwa tamthilia yenyewe iliandikwa katika kipindi cha harakati za kupigania uhuru nchini Kenya, mwandishi hakutuonyesha kwa njia yoyote ile matatizo yaliyowakabili wanajamii, ambayo kwa kweli yalikuwa meingi. Ili kuonyesha kuwa vijana wamezinduka, utafiti huu unadhamiria kuwaonyesha kama washika dau muhimu wanaochangia katika shughuli za kijamii.

Mugambi (1982), katika tasnifu yake, anazihakiki tamthilia zilizochapishwa nchini Kenya tokea 1957 hadi mwaka 1981. Baadhi ya tamthilia zilizokuwa na wahusika vijana ni za Graham Hyslop, Henry Kuria na Gerishon Ngugi. Kulingana na Mugambi vijana katika kazi hizi za mwanzoni katika historia ya tamthilia nchini Kenya, hawakuwa na mchango mkubwa katika kutatua matatizo ya kijamii, kiuchumi wala kisiasa kwa vile madhumuni ya kazi zenyewe, yalikuwa ni kuwatumbuiza wageni.

Maudhui ya mapenzi yaliyomo katika tamthilia hizo za mwanzoni nchini Kenya kama vile: *Kulipa Matanga* (1957), *Nakupenda Lakini...* (1957), *Nimelogwa nisiwe na Mpenzi* (1961), yanawasilishwa kwa nia ya kuwachekesha watazamaji/wasomaji kutokana na mawazo kwamba vijana Waafrika wanasawiriwa kama wakipingaji wa mila zao wenyewe. Mwandishi wa mojawapo ya tamthilia hizi, Henry Kuria, katika utangulizi anakiri kuwa kusudi la kuandika lilikuwa ni kuwatumbuiza wakazi wa Nakuru. Kuhusu *Uasi*, Mugambi anasema kuwa maudhui hayakujengwa ipasavyo, anawaona vijana kama watu wasiochangia katika ukombozi wa mwanamke, kwa vile badala ya John na Raymond kumnusuru Riziki, John anamuoa hata bila mpango kamili.

Suala la vijana linapojitokeza katika tamthilia za Kitsao kama *Uasi* na *Tazama Mbele,* zinaonyesha kushiriki kwa vijana katika maswala ya ndoa na mahusiano ya kimapenzi. Katika tamthilia ya *Tazama Mbele,* kwa mfano walimu wawili ambao ni vijana, wanashirikiana na wanafunzi wao katika mahusiano ya kimapenzi na vitendo vingine vya ukosefu wa nidhamu kama vile mwalimu kumnunulia mwanafunzi uraibu, mizaha ya kiholela na ufadhili wa uavyaji mimba. Tamthilia ya *Tazama Mbele* ni kielelezo cha vijana wasiowajibika kwa njia zozote zile.

Katika tamthilia tulizoziteua, tunakumbana na vijana ambao ni wawajibikaji na wanaojali heshima zao miongoni mwa wanajamii. Vijana hawa wanaonyesha ufahamu wa hali ya juu wa maswala ya kijamii yanayowakabili raia wa jamii zao. Wanapokuwa mawakala wa upinzani, wanadhihirisha kuwa hali zinazokabili jamii ni sugu na zinafaa kubadilishwa kwa mkabala mpya.

Wafula (1999), anazihakiki tamthilia tatu zenye wahusika vijana na maudhui tunayoyatafitia, ambazo ni: *Wakati Ukuta* (1971), *Hatia* (1972) na *Uasi* (1980). Tamthilia mbili kati yazo *Wakati Ukuta* na *Hatia* ni za Ki-Tanzania, *Uasi* (1980) ndiyo pekee ya Ki-Kenya. Kauli yake jumuishi kuhusu vijana ni muhimu sana. Anasema kuwa, vijana huweza kubadilika kwa urahisi kwa vile imani zao za kimsingi zinaendelea kujengeka. Hata hivyo uhakiki huo haukubaini kiwango cha mabadiliko au ufaulu wa vijana katika kuinasua jamii kutokana na matatizo yenyewe. Utafiti wetu unatathmini kiwango cha ufanisi wa vijana katika juhudi za kuleta mabadiliko katika jamii.

Katika uhakiki wa tamthilia ya *Uasi*, Wafula (1999), anaeleza kuwa, mwaandishi wa kazi hii hakuyakuza maudhui yake kikamilifu. Anataja maswala kama *inflesheni na* upangaji uzazi

ambayo Chengo na Katana, wanawe Nyamawi, wanayoyataja kama sababu yao ya kukataa kuoa wake wa pili. Maswala haya hayajakuzwa vizuri wala kuonyeshwi kuingiliana na mfumo halisi wa jamii yao.

Katika uhakiki huu, tunazitambua hizi kama hatua za mwanzoni za vijana katika juhudi za kutambua kwamba, jamii inastahili kuanza kuzitazama upya mila na desturi zilizopitwa na wakati na hasa kutokana na changamoto za maisha ya kisasa.

Kwa maoni yetu, tamthilia ya *Uasi* ni mchango mkubwa katika harakati za kuleta mabadiliko, japo kwa kiwango finyu. Kulingana na nadharia inayotuongoza ya Ki-Foucault, kila jamii huwa na maadili na ukweli wake. Vijana hawa wawili wanabadilisha ukweli aliouamini baba yao wa kuwahitaji kutumia mahari ya dada yao ili kuolea wake wa pili.

Kukataa au uasi wao ni upinzani muhimu sana unaozalisha ukweli mpya kuwa, si lazima waoe wake wengine kwa sababu, tayari walikuwa wameshaoa. Upinzani ni kanuni nyingine ya nadharia ya Ki-foucault, kuhusu uhusiano wa mamlaka ambapo vijana hawa wanabadili fikra na mawazo aliyokuwa nayo baba yao. Hii inawafanya Chengo na Katana wajitokeze kama waasisi wa mabadiliko kwa sababu wametumia maarifa kugundua kuwa, mfumko wa kiuchumi, au *'inflesheni'* haukuwaruhusu kuoa mke wa pili, kwa vile hawangeweza kumkidhia mahitaji yake. Ni kinaya kuwa Nyamawi, badala ya kutimiza mambo ya kimsingi kama kuchimba choo, na kuwakidhi wake zake watatu, anaamua kuyatumia mahari kuolea mke wa nne, na bado aendelee kutarajia kutumiwa msaada kutoka kwa wanawe waliokuwa wamezongwa na tatizo la *'inflesheni'*.

Ni maswala kama haya tunayoyaangazia kwa kuhakiki tamthilia zilizoandikwa hivi karibuni na ambazo hazijahakikiwa kwa mtazamo wetu wa kuwatazama vijana kama maakala wa mabadiliko yenye kuwafaidi wanajamii kwa jumla.

Kutokana na upungufu wa kisanii unaotajwa na wahakiki wa hapo awali wa waandishi kutovikuza vipengele muhimu vya kifasihi katika tamthilia walizozihakikina hasa vipengele vya maudhui na wahusika, ambavyo ni muhimu katika utafiti huu, tumeziteua kazi zilizokuza maudhui changamano na wahusika vijana kiumbuji ili tuweze kupata data ya kutosha katika kuyaafiki malengo ya utafiti wetu.

Mutua (2010), katika tasnifu yake ya M.A., amezihakiki tamthilia tatu akizingatia mitazamo ya vijana katika ukombozi wa mwanamke. Tamthilia alizozihakiki ni: *Kitumbua Kimeingi Mchanga, Migogoro*, na *Natala*. Mutua, amefaulu kuonyesha mitazamo ya vijana kuhusu uhuru wa mwanamke, ambao ni mchango muhimu sana hasa kuhusiana na ukombozi wa mwanamke.

Tofauti naye, utafiti wetu unazingatia kuwa, kwa vile jamii huundwa na makundi mengine yanayoathiriwa na maonevu, kukoseshwa mahitaji na mifumo dhulumati, basi inakuwa muhali kuonyesha kuwa, vijana wanachangia kuwakomboa wanajamii wote wanaodhulumiwa bila kubagua baina ya wanawake, wanaume na watoto.

## 1.8 MBINU ZA UTAFITI

Kimsingi utafiti huu ni uhakiki wa maktabani, hii ni kwa sababu, unahusu kusoma na kuhakiki tamthilia nne tulizoziteua.

Kadhalika tumezipitia tasnifu mbalimbali zinazohusiana na maudhui ya mabadiliko, mapinduzi na zaidi, zinazowahusisha wahusika vijana.

Ili kukuza mada yetu katika mwelekeo kamili, tuliwahoji wataalamu mbalimbali na wasanii waliotupatia mwanga kuhusu maswala mbalimbali yenye kufaidi utafiti huu. Pia,

tumeitembelea mitandao mbalimbali kwenye tovuti, hasa kuhusiana na maswala na dhana ya vijana na nadharia ya Ki-Foucault.

## 1.9 HITIMISHO

Katika sura hii tumezungumzia masuala ya kimsingi yanayohusiana na utafiti huu. Masuala haya ni pamoja na utangulizi wa mada, sababu za kushughulikia mada, tatizo na malengo yake. Aidha tumezungumzia kuhusu misingi ya nadharia na mipaka ya utafiti kuhusu vijana kama mawakala wa mabadiliko katika tamthilia nne tulizoziteua.

# SURA YA PILI

# VIJANA NA MAOVU WANAYOKABILIANA NAYO ILI KULETA MABADILIKO.

## 2.0 UTANGULIZI

Katika sura hii tunayatambua maovu ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Pia tunazijadili juhudi za vijana katika kukabiliana na maovu hayo ili kuleta mabadiliko. Kwanza tumeijadili dhana ya vijana ili kubainisha wahusika tunaowazungumzia. Tumeuonyesha utata uliopo katika kubainisha vijana ni akina nani kulingana na jamii ya Kikenya.

Kisha tumeyajadili maovu yanayosababisha migogoro katika mahusiano ya mamlaka katika tamthilia tunazozihakiki. Aghalabu maovu haya hutokana na viongozi wanaotumia mamlaka vibaya. Viongozi hao, wanapopewa mamlaka na raia, hutarajiwa kuzingatia maadili. Haya ni pamoja na kuhakikisha kuwa kila mwanajamii anapewa haki zake za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Maadili haya hutarajiwa kuzingatiwa katika mahusiano ya mamlaka, hii huhakikisha kuwa pamedumishwa haki, amani na utangamano mwema miongoni mwa wanajamii.

Katika kuyachanganua maovu haya, tumeyagawa katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza imeyaangazia maovu ya kisiasa na jinsi vijana wanavyojitahidi kupambana nayo ili kuleta mabadiliko. Tumejadili mifumo dhulumati na mikakati ya viongozi wasiozingatia maadili ya uhusiano wa mamlaka. Papohapo tumeona jinsi vijana wanavyojizatiti kuhakikisha kuwa maovu hayo yameondolewa na viongozi wenyewe kutolewa madarakani.

Sehemu ya pili imechunguza maovu ya kiuchumi na jinsi vijana wanavyojitahidi kuyaondolea mbali. Sehemu hii imeonyesha usimamizi mbaya wa raslimali za umma na jinsi raia

wanavyotumikishwa bila kufaidi kutokana na raslimali za kitaifa. Hapa maovu kama ufisadi, wizi na kashfa mbalimbali zimepigiwa kachombe.

Sehemu ya tatu imechunguza maovu ya kijamii na jinsi vijana walivyojitahidi kuyabadilisha ili pawe na nafuu katika maisha ya watu walioteseka kwa muda mrefu. Hapa tumejadili jinsi jamii inavyoongozwa kwa njia zisizofaa pamoja na ukosefu wa maadili ya kijamii. Katika maingiliano ya wanajamii, tumeona namna chuki, kiburi na uhasama baina ya makabila zinaweza kuchochea vita hadi kusababisha maafa na hasara kubwa. Hali hizi ndizo vijana wamejitahidi kuziondolea mbali ili pawe na utangamano mwanana katika jamii.

Tumethibitisha kuwepo kwa maovu haya, katika jumuiya ya Wanabutangi katika *Kifo Kisimani,* Wachemwa katika *Pango,* Wandiku na Watange katika *Maua Kwenye Jua la Asubuhi* na Wamonipeyi katika *Seserumbe.* Baada ya kuyajadili maovu katika kila tamthilia, tumeangazia jitihada za vijana katika kupambana nayo ili kuleta mabadiliko yatakayowapa wanajamii matumaini. Katika hali hii, vijana wameweza kujitokeza kama mawakala wafanisi katika kuleta mabadiliko chanya katika tamthilia zote nne tunazozihakiki.

## 2.1 DHANA YA VIJANA

Becker (2011), anaeleza ujana kama kipindi cha mpito toka hali ya utoto hadi utu uzima. Anasema kuwa, hiki huwa ni kipindi ambapo mabadilko mbalimbali hutokea ndipo mtoto awe mtu mzima. Wakati mahsusi ambao mabadiliko haya huwatokea si bayana kwa mtu binafsi kwani jamii tofauti huwa na mitazamo mbalimbali ya kitamaduni kuhusu mabadiliko hayo kwa namna zinavyotambua na kuwapa vijana mamlaka na uwezo wa kimaamuzi. Mitazamo au fasili zenye misingi ya kitamaduni, mila na desturi huzua utata na mkanganyo mkubwa sana katika kuielewa dhana nzima ya vijana.

Erikson, (1961:24) anasema kuwa

> ... ujana ni finomena ya kilimwengu, ambayo huwa ni hali ya kibayolojia lakini inayofasiriwa kitamaduni. Tofauti za ki-umri hutumika kama vigezo vya kimaamuzi katika maisha ya mtu na kwa vile tamaduni ulimwenguni, huwakabidhi watu majukumu kwa misingi ya umri usio sawa ulimwenguni inakuwa vigumu kusema kuwa kuna umri wa vijana kulingana na tamaduni zote ulimwenguni. (tafsiri yetu)

Kitamaduni, fasiri ya vijana yaweza kutolewa kutokana na migao ya kazi walizotengewa, misingi ya kuwapa watu mamlaka na majukumu. Erikson, anatambua majukumu ambayo vijana huhusishwa nayo. Kwa mfano, majukumu ya kijeshi hutengewa vijana kutokana na nishati na nguvu zao za kimwili.

Brown (2002:21), anasema kuwa, dhana ya ujana ni telezi na kwepevu kwa sababu ya utoukubaliano kuhusu maumbile, tamaduni na vipindi vya wakati. Wanaainisha ujana kama kipindi cha maisha kilicho kati ya mwongo wa pili na wa tatu katika maisha ya mtu. Kwa mantiki hiyo ya Brown na wenzake umri wa vijana ni kipindi kilichopo baina ya miaka 11 na 39.

Scott (1999) anasema:

> ...vijana ni watu wenye nguvu nyingi ambazo zinaweza kutumika vizuri au vibaya. Anapendekeza wasipuuzwe kwa vile wana mawazo mapya, nishati nyingi kupindukia na hukabiliana na maswala bila woga au vishawishi vya awali. Wanakabiliwa na changamoto za kutofahamu mambo mengi wanayojihusisha nayo, bila tajiriba na aghalabu hupuuza ushauri kutoka kwa kizazi kikongwe kilichokwisha shuhudia mengi.( tafsiri yetu)

Mamuya (1974), anasema kuwa

> ujana ni ngazi ya maisha kuanzia kubalehe au kuvunja ungo hadi kuwa mtu mzima kamili kuanza miaka 11 hadi 25.

Kutokana na maelezo na ufafanuzi kutoka kwa wataalamu hao, tumemchukulia kijana kama kiumbe mwanadamu aliye katika kipindi cha mpito cha kutoka utotoni na kuelekea utuuzimani ambacho kinaweza kufasiriwa katika misingi ya kiumri.

Kwa vile msingi wa ufasiri wa vijana kitamaduni unaweza kuzua utata mwingi, katika utafiti huu tumetumia ule wa ki-umri ambao kama tutakavyoona pia, una utata wake.

Umoja wa Mataifa, unamweleza kijana kama mvulana au msichana mwenye umri wa kati ya miaka 18 hadi 24. Nayo Jumuiya ya Madola, ambayo Kenya ni mwanachama wake humchukulia kijana kama mtu mwenye umri wa kati ya miaka 16 hadi 29.

Kulingana na Mkataba wa Makubaliano ya Vijana wa Umoja wa Mataifa ya Kiafrika yaani A.U., kijana ni mtu mwenye umri wa baina ya miaka 15 hadi 35.

*Katiba ya Kenya,* (2010) inamtambua kijana kama mwananchi mwenye umri wa kati ya miaka 18 hadi 35.

Kutokana na fasiri hizi tofauti, ni wazi kuwa kuna utata na mkanganyo mkubwa kuhusu ni lini kipindi cha ujana kinaanza na kuishia tunapotumia kigezo cha ki-umri kufasiri kijana ni nani. Kwa mujibu wa tasnifu hii, tumekitumia kigezo cha ki-umri licha ya utata ulioko kwa vile kile cha kitamaduni huzua utata mwingi zaidi. Tumetumia mseto wa viwango vya umri vilivyowekwa na Mkataba wa Makubaliano ya Vijana wa Umoja wa Mataifa ya Kiafrika yaani A.U. miaka 15-35 na katiba mpya ya Kenya ya mwaka wa 2010 ambayo inaweka vijana kama watu walio kati ya umri wa miaka 18-35. Hii inaturuhusu kuchukuwa kiwango cha chini baina ya hizi mbili ambayo ni miaka 15, na kile cha juu ambacho ni sawa kubaki hivyo, yaani miaka 35. Kwa kufanya hivyo, tumefasiri vijana kama viumbe wa kiume au kike walio kati ya umri wa miaka 15 hadi 35.

Vilevile tunakichukulia kipindi cha ujana kama kinachokumbwa na mabadiliko ya kimwili, kiakili, kisaikolojia, kimtazamo na kivitendo.

Katika tamthilia tulizoziteua, tunawatambua wahusika vijana kutokana na maelezo ya waandishi. Pale ambapo hatukubainishiwa umri kamili, tumeukadiria kutokana na maingiliano au maneno ya wahusika wengine katika mahusiano baina yao.

## 2.2. MAOVU YA KISIASA

Maovu ya kisiasa ni yale yanayohusiana na mifumo ya serikali zilizochaguliwa na raia na yanayofanywa na viongozi walioteuliwa katika nyadhifa serikalini. Hii ni kutokana na hali za raia kuwapa mamlaka viongozi kwa njia za uchaguzi. Kwa njia hii, raia huwaruhusu viongozi kufanya maamuzi kwa niaba yao kuhusu raslimali za kitaifa, uchumi, sheria, uteuzi wa viongozi katika asasi na mashirika mbalimbali ya kitaifa.

Maovu ya kisiasa, yanahusu matumizi mabaya ya mamlaka, maamuzi mabaya, ustawishaji wa mifumo dhulumati, mauaji kutokana na migogoro ya kisiasa na hila zozote zenye kuwadhuru raia waliowapa viongozi hawa idhini ya kuwaongoza. Sehemu ifuatayo imejadili maovu haya kama yanavyojitokeza katika tamthilia zote nne.

### 2.2.1 UDIKTETA

Kirkpatrick (1982) anasema kuwa:

> ...mhimili wa udikteta ni kiongozi wa kimabavu, ambaye hujionyesha kama anayeweza kuamua hatima ya watu wote ambao wamepofushwa na kufikia kiwango cha kutofikiria. [dikteta] pekee hujichukulia kuwa ndiye anayejua kile ambacho watu wengine wote wanataka au kuhitaji. (Tafsiri yetu)

Kamusi sanifu, (2006) inafafanua kuwa;

> ...udikteta ni aina ya uongozi ambapo mtu hutawala nchi kwa amri yake peke yake bila kushauriwa. Dikteta anaweza kuchukuliwa kama mtu mwenye tabia ya kutaka lifanywe jambo lile analosema bila ya kupingwa

Kulingana na Wikipedia, (2012)

> Udikteta ni uongozi wa mtu mmoja, au kundi dogo la watu ambao hawazingatii sheria, katiba wala matakwa yoyote ya kijamii au kisiasa. (tafsiri yetu)

Kutokana na fasiri hizi, tasnifu hii imeuchukua udikteta kama aina ya uongozi ambapo mtu mmoja hujikweza na kufanya maamuzi peke yake. Pia hufanya maamuzi kwa kuwapuuza raia

kana kwamba, hawakuchangia katika kumuidhinisha uongozini. Hali hii huwaumiza wanajamii kwa kiwango kikubwa. Ni bayana kuwa kiongozi wa aina hii huwa amekiuka maadili ya mahusiano ya mamlaka. Anapochaguliwa hutarajiwa kufanya maamuzi kama mwakilishi wa umma anayestahili kuwahusisha raia kwa kiwango kikubwa ili kuwatosheleza na kuwaridhisha kulingana na kanuni zilizokubaliwa kisheria na kikatiba.

Katika tamthilia tulizoziteua, tumeonyesha jinsi madikteta wanavyowaumiza raia wanaowaongoza. Viongozi wanaendelea kuongoza kimabavu na kuzua woga hivi kwamba kuna pingamizi ndogo kutoka kwa watu wazima. Ni katika hali hii ambapo vijana wanajitokeza kikakamavu na kuzua upinzani unaoongozwa na ufahamu mpana wa dhuluma wanazotendewa wanajamii. Lengo la vijana hawa ni kuwazindua wanajamii wafahamu kuwa hali inaweza kubadilika ikawa bora iwapo wataungana na kudai haki zao, au kuwaondoa viongozi waovu kutoka mamlakani.

Udikteta umejitokeza wazi katika tamthilia tunazozihakiki kama tutakavyojadili katika sehemu ifuatayo.

Katika *Kifo Kisimani,* Bokono anajitokeza kama dikteta kama anavyowaongoza Wanabutangi. Kuna ushahidi mkubwa wa ukandamizwaji wa raia wake. Wanabutangi wamenyimwa haki zao za kutumia raslimali zilizopo Butangi. Bokono pamoja na vikaragosi wake wamejilimbikizia nyingi za raslimali hizi kama vile visima vya maji, bonde la kulishia mifugo na ubinafsishaji wa viwanja vya umma.

Bokono anaamini yeye ni kiongozi aliyeteuliwa na Mungu badala ya raia. Hii inakiuka kanuni za mahusiano ya mamlaka kwani tunatarajia kuwa mamlaka ya Mtemi Bokono yametolewa kwa hiari na raia wote alipoidhinishwa kuchukua mamlaka ya kuwawakilisha. Kauli ya Bokono inadhihirisha udikteta wake anaposema:

> ...Uongozi wangu hutoka kwa Mungu.
>
> Mamlaka yangu yametoka juu.
>
> ***Mungu aliniketisha kwenye kiti*** cha enzi
>
> cha Butangi...(uk 10, msisitizo ni wetu)

Hii inaonyesha kuwa Bokono hakuuona umuhimu wa kuwatumikia Wanabutangi kwa sababu kulingana naye, sio wao waliochangia katika kuyapata mamlaka aliyo nayo.

Mwelusi, kijana mwenye umri wa miaka 24, anatambua kuwa japo Bokono ni kiongozi mwenye nguvu, ana upungufu wa kutoweza kufanya mambo fulani. Mwanzoni mwa tamthilia, Mwelusi anasema kuwa Bokono hana budi kujikinga kutokana na miale ya jua kali kwa sababu hana mamlaka dhidi yake. Inambidi ajenge kibanda kujisetiri ili jua lisimuuguze. Kwa hivyo hata kama yeye ni kiongozi kuna nguvu zingine azinyenyekeazo na kuziogopa kwani yeye ni mwanadamu kama wengine. Mwelusi anaonyesha kuwa Bokono ni dikteta kwa watu Wanabutangi anaposema:

> ...hawezi kulionya jua
>
> Hawezi kuliambia kwamba likichomoza litaona cha mtema
>
> kuni...(uk 1)

Ugunduzi huu ni muhimu kwa sababu unajenga msingi wa upinzani dhidi ya Bokono kwa kutilia maanani kuwa yeye ni mtu katili anayetumia vitisho kwa watu.

Mwelusi anaelewa kuwa mgogoro uliopo kuhusu uongozi wa kiimla unaweza kutatuliwa iwapo vijana wataweza kushirikishwa. Hii ndio maana anamwambia Kaloo kuwa katika wakati wa vita, vijana hupigana kwa niaba ya umma ulionyanyaswa.

Mwelusi pia anatambua uongozi usiojali maslahi ya Wanabutangi na ambao umekuwepo tangu enzi za Mtemi Mrima, na unafaa kuondolewa mbali. Hii ndio sababu Mwelusi anakariri imani hii akisema:

> …sio nia yangu au ya wazalendo wenzangu kuvuruga
> amani katika Butangi. Ndoto yetu ni kuona kwamba kuna
> uhuru na heshima kwa kila Mwanabutangi.( uk. 32-33)

Mwelusi anamweleza Batu kuwa wazalendo wa Butangi walikuwa na imani kuwa maovu kama vile vitisho, utawala mbaya, utumiaji nguvu, umwagaji wa damu yangeondolewa mbali ili Butangi pawe mahali salama kuishi.

Mwelusi anawaona viongozi waliopo Butangi kama nzige hatari wanaolemaza na kuharibu rasilimali zote wakiongozwa na Bokono katika kutozingatia kanuni zilizowekwa. Anaongezea kuwa japo kuna tofauti za mila na tamaduni miongoni mwa Wanabutangi, tatizo kubwa ni viongozi ambao wanawapendelea baadhi ya watu.

Katika tamthilia ya *Seserumbe*, tunamtambua waziri Seserumbe kama dikteta wa wizara ya Utandawazi, Uchukuzi na Teknohama. Seserumbe ni kiongozi anayewaamrisha wafanyakazi katika wizari husika kimabavu. Tunamwona akimlazimisha Kembo kuandika hundi ya malipo kwa *Acme Contractors* bila kuzingatia kanuni na taratibu za utendakazi. Vilevile Seserumbe anamwamuru Kembo kumlipa yeye kiasi kikubwa cha pesa akitumia bajeti iliyotengewa vibarua na waliokuwa wameomba malipo-awali kwa kugharamia mahitaji yao ya dharura. Maamuzi yanathibitisha umabavu wake anaposema:

> … mimi ndiye waziri katika wizara hii, na waziri
> kama hujui ni ***rais wa wizara***! Nafasi yangu
> inaniruhusu kupata posho ninayotaka na wakati

ninapoitamani... wale ni watu wanaojua kungojea... ( uk. 28. Msisitizo ni wetu.)

Kembo ni kijana na ndiye mhasibu mkuu katika wizara hii. Anajitahidi kuzua upinzani ili kubadilisha hali ya kidikteta iliyopo wizarani. Kembo anapotambua kuwa waziri anataka mambo yafanyike atakavyo bila kujali haki za wafanyakazi, anaamua kutumia maarifa yake kuwatetea na kuwaokoa watu dhidi ya udikteta wa Seserumbe.

Kembo anamtahadharisha Seserumbe dhidi ya kuivunja mioyo ya wafanyakazi kwa kupanda mbegu ya uhasama. Hii ni kutokana na hali kuwa, wafanyakazi wa daraja za chini hawajaongezwa mishahara ilhali wakubwa wao walikuwa wameongezwa mara tatu. Vilevile posho la usafiri nje ya vituo vya kazi ilikuwa imepunguzwa kwa wafanyakazi wao hao. Kembo anamtahadharisha Seserumbe dhidi ya kutaka mambo yafanywe kulingana na mapenzi yake, badala yake, anampendekezea kuwa kanuni na taratibu za utendaji kazi zifuatwe ili kudumisha uadilifu. Kembo anamtahadharisha waziri kwa methali kuwa 'sisimizi huweza kumuua ndovu' na 'kisu huvunjikia bogani'. Methali hizi zinamaanisha kuwa Seserumbe kwa kujikweza kama kiongozi asiyejali, huenda siku moja aporomoshwe na hao wafanyakazi wa ngazi ya chini.

Kuporomoka huku hatimaye, kunatokea wakati Kembo anamshinda Seserumbe katika uchaguzi. Mabadiliko makubwa yanatokea na kumdhoofisha Seserumbe ambaye hakutaka kuamini kuwa alikuwa ametibuliwa kutoka madarakani. Kembo anaweza kuzifichua kashfa za Seserumbe za ulanguzi na kutozingatia maadili kazini. Wakaguzi wanatambua matumizi mabaya ya pesa wizarani kama Kembo alivyokuwa akimtahadharisha waziri.

Baada ya Kembo kuchaguliwa kama mbunge na kuwa waziri, kunaanzishwa uchunguzi unaoletea kushtakiwa kwa Seserumbe kujibu mashtaka ya matumizi mabaya ya mamlaka alipokuwa waziri. Hali ya kuondolewa uongozini ikifuatiwa na barua ya mashtaka, ndizo zinazomfanya kupatwa na kichaa na kudhoofika afya.

Udikteta katika tamthilia ya *Pango* unajitokeza kupitia kwa Ngwese ambaye ni kiongozi wa pango la Wachemwa. Anatumia mamlaka aliyopewa vibaya ili kujinufaisha akiwa kwenye kigoda cha uongozi wa pango. Vilevile alikuwa ameshiriki katika kashfa ya ufisadi hapo awali alipokuwa mkurugenzi katika shirika la umma.

Ili kujidumisha katika uongozi, Ngwese anatumia mabavu na vitisho. Hili linajitokeza wazi katika kampeni za uchaguzi wa kiongozi wa pango. Ngwese anapoona kuwa anakabiliwa na upinzani mkali kutoka kwa Katango, anatumia hila, mabavu na vitisho ili kumtia woga Katango asidhubutu kuendelea kuwania uongozi.

Katango, kijana ambaye ni mwalimu anachangia pakubwa katika kumtambulisha Ngwese kama dikteta. Anatufahamisha kuwa huyu ni kiongozi aliyekuwa na historia ya usaliti. Ukweli tumaoufahamu kupitia kwa Katango unaeleza kwamba, babu yake Ngwese alikuwa msaliti aliyeshirikiana na wakoloni katika kulipora pango. Hii inamaanisha kuwa Ngwese alikuwa na maruweruwe ya ukoloni mkongwe na hivyo hangeweza kuwaongoza watu kwa kujitolea. Alitaka kuwaongoza watu kimabavu ili aendeleee kufaidi kutokana na mataifa ya kigeni. Hii ndiyo maana anamtolea Katango vitisho vya kikatili iwapo ataendelea kupingana naye.

Katango analifuatilia jambo hili kwa kuhakikisha kuwa Wachemwa wamemfumania Ngwese akishirikiana na wakoloni wakongwe wakiirina asali pangoni. Ushahidi wa usaliti kwa wageni unapatikana kutokana na malipo ya fedha za kigeni alizozipokea kama vile Dola, Pauni, Yuro na Yeni. (Uk 79)

Jitihada za Katango za kutaka mabadiliko ndizo zinazomfanya Ngwese kuwatumia wahuni na waganga kumtia Katango kitata asiweze kunena na kuwafahamisha raia ukweli wa mambo.

Kulingana na mihimili ya nadharia ya Ki-Foucault, huwa kuna mikakati kutoka pande mbili. Mikakati ya upande wa kwanza huwahusisha viongozi wanaojitahidi katika kujidumisha katika madaraka. Upande wa pili huhusu mikakati ya wanaoongozwa. Hawa huzua upinzani pale wanapohisi kwamba mamalaka waliyoyaidhinisha hayazingatii maadili.

Kutokana na ukweli huu, tunaichunguza mikakati inayotumiwa na viongozi wa kidikteta kama walivyosawiriwa katika tamthilia nne tulizoziteua, kisha tunaona namna vijana wanavyozua upinzani kwa kusudi la kuleta mabadiliko chanya yenye kuwanufaisha wanajamii wanaoumia katika mahusiano ya kimamlaka.

#### 2.2.1.1 MKAKATI WA KUWATUMIA ASKARI MAKATILI

Katika tamthilia ya *Kifo Kisimani,* askari wanaohudumu Butangi wanatumiwa sio kwa kudumisha usalama wa raia, bali kumlinda Bokono na maslahi yake. Hii ndiyo sababu askari II na III wanamtuhumu na kumpoka Mwelusi chakula alicholetewa gerezani. Vilevile wanatishia kumdhulumu Andua na Atega.

Askari II, anatujuza kuhusu sababu zake za kumwombea Bokono kubakia madarakani. Tunaufahamu ukatili wake alipokuwa katika kikosi kingine. Hii ilitokea wakati yeye na wenzake walipomtesa mshukiwa mmoja hadi akafa. Anaeleza walivyomtesa mtuhumiwa huyo kwa kumfinya sehemu zake za siri, kumng'oa kucha, kumpiga kinyama hadi kumuua na hatimaye, kumzika kisiri mwituni.

Hii inatuonyesha wazi kuwa askari hawa walikuwa chombo cha kuendeleza udikteta wa Bokono. Walifanya hivi kwa kutoa vitisho na kueneza woga ili kuhakikisha kwamba hapakuwepo na upinzani wa aina yoyote dhidi ya Mtemi Bokono.

Ukatili zaidi unadhihirika tunapowaona askari wakiwahujumu raia na hata watoto wadogo. Tunaambiwa katika uk 50 kwamba, walimng'oa meno mtoto wa Chendeke na baadaye askari wao hao wakamjeruhi Andua usoni alipokwenda kuteka maji katika kisima cha Mkuyuni.

Mwelusi anendelea na harakati za mapinduzi hata alipokuwa gerezani. Kitendo chake cha kuikereza minyororo na kutoka gerezani kinaonyesha kuwa askari hawangeweza kuyazuia mabailiko aliyoyanuia pamoja na raia wazalendo waliomuunga mkono. Kwa hakika, tunauona ujinga wa askari wanaposema kuwa walikuwa wameipeleka mikuki yote ikanolewe.

Atega rafikiye Mwelusi, anatudhihirishia ubunifu wa vijana. Kijasiri anaandaa mpango wa kumwokoa Mwelusi kutoka gerezani kwa kuutumia ujanja wa kuwaletea askari tembo. Kwa kuielewa tabia yao ya kupenda vitu vya bure, anawatega kwa tembo ambayo wanakunywa na kulewa chakari wasiweze kulinda doria. Upumbavu wao pamoja na ulevi unafaulisha mpango wa kumtorosha Mwelusi kama anavyosema:

> ...Atega aliniletea tupa ikiwa ndani ya mkate wa wishwa. Aliwaletea askari tembo... (uk 82)

Askari wakanasika kwa kufakamia tembo iliyokuwa kwenye kikapu cha Atega. Walipolewa, Mwelusi aliendelea kukereza minyororo hadi pale umati wa wazalendo ulipofika na kulifungua lango la gereza na kumwezesha kutoroka.

Baada ya Mwelusi kutoroka gerezani, askari hawa wanaingia matatani kwa kushindwa kueleza njia alizozitumia kutorokea. Tunaona kuwa Mwelusi, Atega na Andua, wanaweza kutekeleza mambo mengi kwa kipindi kifupi kwani askari hao hawakuweza kuwapata hata walipokwenda kisimani kuvunja sheria machoni mwa Zigu ambaye hakumtambua Mwelusi. Vijana hawa walikuwa tayari kuwaongoza Wanabutangi wapenda mabadiliko katika harakati za kujikomboa kutoka kwa uongozi wa mabavu ya Bokono na askari wake wakatili.

#### 2.2.1.2 MKAKATI WA KUWATUMIA MAKACHERO

Katika tamthilia ya *Kifo Kisimani,* tunakumbana na makachero wawili wakatili, Mweke na Talui. Wawili hawa wanajitokeza kama vyombo vya kudumisha udikteta wa Bokono. Hii inadhihirika wanapowasukuma Kaloo, Azena na Gege kwenda kuhojiwa na kueleza kilichosababisha ususiwaji wa mahudhurio ya mkutano wa Bokono, mwanzoni mwa tamthilia. Makachero hawa ndio waliomkamata Mwelusi na kumpeleka gerezani. Hapo ndipo tunapoushuhudia ukatili wao wakimtesa kwa pamoja huku wakimbeza na kumwita 'Mtukufu Mtemi'. Wanamtuhumu Mwelusi kuwa kiongozi wa kundi la wahuni lililojulikana kama Kabakaba. Kutokana na maagizo ya Batu, wanamtesa Mwelusi kikatili ili wamtishe hadi akiri kuwa yeye ndiye aliyekuwa amewachochea raia wa Butangi ili kuususia mkutano.

Mwelusi kama mwanamabadiliko, anajikaza kutofichua siri yoyote kuhusu mipango ya kuleta mabadiliko licha ya kichapo na mateso aliyoyapokea kutoka kwa makachero Mweke na Talui. Ujasiri wake ni ishara ya ukakamavu katika imani kwamba, yu radhi kujitolea mhanga yapatikane mabadiliko yatakayowafaidi Wanabutangi.

Mweke na Talui ndio wanafanikisha hila za kumuua Mwelusi kwa kumhadaa Gege ili amsaliti nduguye. Hadaa hii inapangwa kwa kumwahidi Gege kuwa, iwapo angekubali kumuuwa Mwelusi, basi angeozwa Alida bintiye Bokono. Gege anahadaika kwa urahisi kwani

alitamani kumwoa mke mzuri na kama walivyomwambia makachero, Alida alifanana na hurulaini ambao ni wazuri ajabu. Vilevile anaahidiwa harusi ambayo ingedumu muda wa siku kumi pamoja na utajiri mzomzo.

Kifo cha Mwelusi hakikuwa mwisho wa harakati za kudai mabadiliko. Mapambano ndiyo sasa yalichacha. Atega rafikiye Mwelusi, alihakikisha kuwa wazalendo wote wameyaendeleza mapambano hadi kuyafanikisha.

Katika tamthilia ya *Pango* tunawaona makachero, waliotumiwa na Ngwese kupoteza ushahidi na kumwondolea tuhuma zilizokuwepo kuhusu upunjaji wa pesa katika shirika la umma. Hii inamaanisha kuwa, makachero walikuwa wakitumiwa ili kuficha ukweli kuhusu maovu ya viongozi.

Katango alilifuatilia jambo hilo licha ya ushahidi huo kufutiliwa mbali. Anahakikisha kuwa ukweli umejulikana kwamba Ngwese alitumia cheo chake vibaya kwa kulipora pango akiwa na wenzake. Kufaulu kwa Katango kunatokea pale Wachemwa wanapowafumania Ngwese na wenzake wakijitayarisha kurina asali kisiri. Hapo wanatiwa nguvuni.

**2.2.1.3 MKAKATI WA KUWATUMIA WASHAURI MAKATILI**

Bokono alikuwa na washauri watatu; Batu, Zigu na Kame. Kati yao, Batu na Zigu walikuwa makatili na waliotumika kuuendeleza udikteta. Matendo yanayowadhihirisha kuwa wakatili ni pamoja na kupanga na kumzuilia Mwelusi gerezani bila kumfanyia mashtaka ya kisheria, kupanga njama ya kumuua na kuyatekeleza mashambulizi katika kijiji cha Bulusi.

Vilevile, Batu na Zigu kwa ukaragosi wao uliokithiri, wanachangia pakubwa katika kuuendeleza udikteta wa Bokono. Tabia yao ya kumsifu Bokono na kumdhihirisha kama

kiongozi aliyeteuliwa na Mungu, na atakayeongoza Butangi kwa miaka mia, inakichochea kiu chake cha kuongoza kimabavu ili utabiri wao utimie. Kwa mfano, Zigu na Batu wanaposema:

> Zigu : Mungu mwenyewe alikuketisha kitini.
>
> Batu: Utaendelea kuongoza Butangi kwa manufaa ya
>
> Wanabutangi wote.
>
> Zigu: Utaongoza Butangi kwa miaka mia moja.(uk 10 )

Washauri hawa pia ndio wanaotekeleza marufuku gandamizi zilizotangazwa na Bokono. Marufuku yaliyokwishatangazwa ni pamoja na matumizi ya kisima cha Mkomani na uchungaji katika bonde la Ilangi. Mfano mzuri wa utekelezaji wa kanuni hizi ni pale Zigu alipowafukuza Andua, Atega na Mwelusi wasiteke maji kisimani huku akiwaonya na kuwatishia:

> …nimesema msidhubutu. Msinilazimishe. Msinione umri wangu mkanidharau. Simba mzee bado ni simba…niko tayari kutetea kanuni za Butangi…hasa kwa silaha. (uk 94).

Batu anajidhihirisha kama mshauri katili. Hii inajitokeza pale anapowaamuru makachero kumpiga Mwelusi hadi akiri kuwa kiongozi wa kundi la wahuni la Kabakaba. Baada ya kuteswa na makachero, Batu anajitokeza na kumwahidi jinsi ambavyo angetunukiwa mamlaka ya uongozi wa vijana, kupewa ardhi nzuri na ngombe iwapo angejitokeza katika mikutano ya hadhara na kukiri kuwa alikuwa ameacha kuwachochea raia. Batu anamtolea Mwelusi vitisho vikali iwapo hangekubali kukiri uchochezi, anaposema;

> …naona nikupe fununu ya ukweli.

> Kujaribu kuvuruga amani katika Butangi
> kuna hatari. Na kuna hatari hata kubwa zaidi
> kukataa kuomba msamaha baada ya kushiriki
> katika kosa hilo... (uk 32)

Washauri hawa wanaendelea kupanga jinsi watakavyomuua Mwelusi, mapendekezo yao ni kuwa apigwe 'pembe ya faru' au ajali ya kulazimishwa. Hii inadhihirisha ukatili wao.

Tunaziona jitihada kubwa za vijana katika kukabiliana na washauri hawa. Kwanza, wanahakikisha kuwa, hawakuhudhuria mkutano ulioandaliwa uwanjani. Tunamwona Mwelusi akitangulia uwanjani palipopangiwa kufanyika mkutano ili kuhakikisha kwamba, hakuna mtu yeyote kati ya wazalendo wapenda mabadiliko waliohudhuria mkutano wenyewe. Vilevile vijana kama Andua, Mwelusi na Atega wenyewe wametangulia kabla ya wazalendo wengine kufika siku walipomkuta Zigu.

Mwelusi vilevile hakubabaishwa na vitisho vya Batu alipomtaka kutubu uchochezi kama kiongozi wa kundi haramu la Kabakaba. Mwelusi anaitakidi:

> Butangi ni kubwa kuliko Mtemi yeyote.
> ....Wanabutangi hawatabaki kwenye
> usingizi.( uk 33-34)

### 2.2.1.4 MKAKATI WA KUTUMIA GEREZA NA VITISHO

Katika *Kifo Kisimani,* Mwelusi amezuiliwa gerezani. Gereza lenyewe limesawiriwa kama mahali palipojengwa ili kufanikisha mateso kwa yeyote aliyeupinga uongozi wa dikteta Bokono. Taswira ya ukatili inatokeza vyema tunapoambiwa katika maelekezo kuwa:

*Kilikuwa ni chumba chenye kidirisha kimoja, kuta na sakafu chafu, upande mmoja kuna mlango mzito....mlio wa kite....pingu mikononi... ana jeraha. Damu inavuja kutoka jeraha hilo Mweke anamsukuma* (uk 21)

Gerezani ndiko kunakoendeshewa mateso kwa wanaojaribu kuupinga uongozi wa Bokono. Makachero Mweke na Talui wanampiga Mwelusi kinyama bila hata kujali iwapo alikuwa kweli ameshiriki uchochezi au la.

Mateso haya yanaendeshwa kwa ushirika wa makachero na amri ya Batu ambaye ni mshauri mkuu wa Bokono. Kazi ya makachero ilikuwa ni kumpiga Mwelusi na kumtia woga hadi akiri kwamba, yeye ni mchochezi na kiongozi wa kundi haramu la Kabakaba.

Batu alifuatia kwa vishawishi na vitisho. Ahadi yake ilikuwa kwamba Mwelusi angetuzwa na kuteuliwa kama kiongozi wa vijana, apewe ardhi na mifugo iwapo angekiri kuwa mchochezi aliyeongoza kikundi haramu cha Kabakaba. Anapoona kuwa Mwelusi ana msimamo thabiti wala hatetereki, anamtolea vitisho vikali.

Baadaye, tunakumbana na askari wawili makatili katika gereza alikozuiliwa Mwelusi. Hawakujali iwapo mfungwa alitiwa gerezani kwa kuwa na hatia au la. Wanaendeleza ukatili wa kigereza kwa kufanya mambo bila udadisi wowote.

Askari hawa pia wanajihusisha na kashfa ya kumpoka Mwelusi chakula hivyo kumtesa kwa njaa. Kila Mwelusi alipoletewa chakula, walikichukua kwa kusingizia kumpelekea, kisha walikila wenyewe. Hapo hapo waliwatolea Andua na Atega vitisho vya kimapenzi au kipigo walipoleta chakula gerezani. Kwa mienendo yao mibovu, tunaweza kusema kuwa askari hawa walikuwa vyombo vya kidikteta, wakawa mawakala wa kueneza dhuluma na kuwaogofya raia wa Butangi.

Mwelusi anapotoroka kutoka gerezani tunatambua kwamba yuko tayari kuendeleza harakati zake za kuleta mapinduzi. Anapotoka gerezani anamwambia mamake kuwa:

.... La! Sitatoroka, Mama.

Butangi sasa inawahitaji wazalendo wake kuliko nyakati za nyuma. Tunao mpango kabambe... Watu wengi watakutanika huko... huu utakuwa mwanzo wa mwisho. (uk. 83)

Vitisho vilitolewa kwa njia mbalimbali. Kulikuwepo na vitisho vilivyotolewa kwa mtu binafsi au kuelekezwa kwa umma. Katika *Kifo Kisimani,* Mwelusi alitolewa vitisho kibinafsi kutoka kwa washauri na makachero wa Bokono. Batu anamwonya Mwelusi dhidi ya kuendeleza uchochezi wake. Vitisho hivi tumevijadili katika mkakati wa washauri wakatili hapo juu.

Vitisho kwa umma vinatokea wakati serikali ya Bokono inapopanga na kushambulia kijiji cha Bulusi. Hili lilifanyika ili kuwatia watu woga. Serikali ya Bokono ilitaka wanakijiji hao wahisi kuwa walikuwa hawana budi kumuunga mkono Bokono la sivyo hangewasaidia iwapo mashambulizi kama hayo yangetokea. Haya tunayajua kupitia kwa maneno ya Azena anaposema mashambulizi yalitekelezwa na:

... wahuni wa kulipwa....

kuwatia watu uoga ili waendelee kuimba nyimbo za kumsifia Mtemi... ( uk 81)

Katika tamthilia ya *Pango,* Ngwese anatumia wahuni waliojivika nyuso wasitambulike ili kuwashambulia na kuwatolea vitisho Katango na Kibwana dhidi ya kumpinga Ngwese katika uchaguzi. Katika onyesho la tano, tunashuhudia ukatili kwa jinsi Kibwana anavyopigwa kutoka nyuma na kuanguka. Kisha wale washambulizi wawili wanaendelea kumhangaisha Katango kwa kutishia kumdhulumu kimapezi iwapo hatakoma kumpinga Ngwese katika kampeni kama wanavyosema:

…Sikiliza kirukanjia wewe! Tangu leo ukome,

Unasikia? Usijitie kumpinga Mzee….usipokoma

hata tutaku….(uk 32)

Katika kampeni za kumchagua mlinzi wa pango, Ngwese anajidhihirisha kama kiongozi ambaye atatumia mbinu zozote kuongoza kama anavyosema :

Ndimi kimbunga nipigaye,

Ndimi tufani nifagiyaye,

Ndimi dhoruba nifagiyaye,

nani wa kunitangua ?

kijana ? ( uk 48 )

Katika kauli hii Ngwese ametumia jazanda angamizi kama vile; kimbunga, tufani na dhoruba kudhibitisha kuwa uongozi wake unatarajiwa kutumia mabavu kwa kiwango kikubwa. Hii inajitokeza kama kitisho kwa Katango na pia umma mzima utakaoongozwa na Ngwese.

Ngwese anaendelea kumtisha Katango kwa kudhubutu kumtajia ukweli kuhusu historia ya familia yake kwamba, babu yake Ngwese, alikuwa msaliti. Hii ni kutokana na mienendo yake ya kushirikiana na wakoloni na kuwasaliti waliopigania kuikomboa jamii yao. Jambo hili linamghdhabisha Ngwese anayefahamu fika kwamba, Katango anamaanisha kuwa yeye ni msaliti vilevile. Ndiyo maana akatoa vitisho vikali alipomwambia Katango;

Basi nitakunyamazisha mimi

…Kuna siku itakuchea… siku hiyo utajuta

…Mimi ni kimbunga, subiri tu. (uk 14 )

Baada ya kutambua kuwa Katango hakuwa tayari kuacha upinzani hata baada ya kushindwa katika uchaguzi, anaamua kutumia njia katili zaidi za kumtia kitata asiweze kuzungumza. Ni

bayana kuwa Ngwese anamwogopa Katango ambaye anaelewa ukweli kuhusu nani wanaochezea pangoni. Ni kwa sababu hii ambapo Ngwese anamfanyia Katango uganga huku akinuiza maneno yafuatayao:

> …vinywa vyao vyepesi
>
> Vizibwe na kufumwa…
>
> Isitoke kauli hata moja
>
> Wasije wapotosha wengine
>
> Ndimi zao kali zitahirishwe…
>
> Wawe mithili ya vizuu…(uk 62)

Vitisho zaidi vya Ngwese, vinajitokeza pale anapomkemea Kauleni. Huyu alikuwa mmoja wa waungaji mkono wake aliyekuwa amehama kambi na kuanza kumuunga Katango mkono. Anatishia kuiporomosha biashara ya Kauleni kwani Ngwese ndiye aliyemfadhili kwa kumpatia kiwanja cha kujengea hoteli, na kumtafutia liseni ya kuendesha biashara hiyo kama anavyomtisha:

> … ukienda kinyume si unajua, unyoya wa maisha ni mrefu; Nami nitakuwa na fursa yangu. Hamna haja ya kusema kutatokea nini…ukichezea sega la nyuki, jiandae kutafunwa… (uk 30 ).

Katika tamthilia hii, Katango anampinga Ngwese katika kila hatua ya vitisho vyake. Anamweleza kuwa kipindi cha ubabedume wa kumtazama kama mwanamke na kijana kimepita na anafaa kujua kwamba watu sasa wanafahamu mambo mengi.

Katango anaposhambuliwa ili kumtia woga, anakabiliana na wavamizi waliotumwa na Ngwese. Anamuuma mmoja na kumpiga mwenzake huku akiwaita waoga na wanyama makatili (uk 33).

Anawaeleza wapiga kura kwamba, Ngwese ni mzee anayefaa kurudi nyumbani na kuwaachia vijana uongozi kwa vile alishindwa na kazi aliyopewa. Anaendelea kusema kuwa vijana ni watu wanaotumia akili badala ya mabavu ayatumiyao Ngwese. Kulingana na Katango vijana ni moyo wa pango na wanatarajiwa kuleta matumaini ya jamii ya baadaye (uk 42)

Hata baada ya mashambulizi na kushindwa katika uchaguzi uliokumbwa na ufisadi, Katango anaendeleza juhudi zake. Anawahimiza vijana wenzake kutoghairi nia waliyokuwa nayo mwanzoni ya kuleta mabadiliko. Pia anawaonya dhidi ya kupumbazwa na vishawishi alivyotoa Ngwese ili kuwahimiza kumpigia kura. Katango anang'ang'ania ukweli ujulikane kwamba Ngwese alikuwa mnafiki aliyetumia vitisho ili kuzuia kujulikana kuwa alishiriki ufisadi, usaliti na maovu mengineyo.

Katika tamthilia ya *Maua Kwenye Jua la Asubuhi,* watu kutoka kabila la Watange wanawatisha Wandiku kwa njia ya barua. Katika mojawapo ya barua hizo, watu waliokuwa wakijiita 'mashujaa wa Watange', wanawaonya Wandiku kuwa iwapo wangepuuza wito wa kuondoka Loloma Kaskazini, basi wangejutia kuzaliwa kwao.

Mmoja wa mababe wa vita na kiongozi wa kabila la Watange anayeitwa Chebwe, alikuwa na mazoea ya kutoa vitisho. Vitisho vyake vya kwanza anavielekeza kwa Toiche. Huyu alikuwa kijana Mtange, aliyepewa kibarua cha kuinunua mishale. Toiche anaufanya uamuzi huu pale anapogundua uongo katika kiapo alicholishwa kuwa Watange walikuwa wanapigania haki za kabila lao. Anafahamu kuwa viongozi walikuwa wakiwatumia vijana ili kuzifanikisha ndoto

zao. Kwa hivyo, anaamua kujitenga na maandalizi ya vita. Hapo ndipo Chebwe anamtishia maisha yake kwa kukikiuka kiapo cha kikabila.

Vitisho vingine vya Chebwe vinaelekezwa kwa kabila la Wandiku. Ni katika vitisho hivi tunapogundua ukatili na maafa yanayonuiwa kutekelezwa. Chebwe anasema kuwa watawapiga Watange, kuwachinja kwa kila namna, kuwalipua miguu kwa mabomu ya kutega ardhini na mengine mengi kama anavyosema:

> ....Wanacheza na moto. Watalilia Msalaba Mwekundu mpaka machozi yao yawe mekundu kuliko msalaba wenyewe...Tutawashinda kwa mamna ambayo hawatasahau kwa miongo mingi.
>
> (uk 62 )

Vijana katika tamthilia hii wanakataa kuathiriwa na vitisho hivyo. Tunawaona Waito na Nali wakishirikiana kwa urafiki mkubwa. Urafiki huo wao unawakasirisha Chebwe na Kabitho waliojaa chuki za kikabila.

Waito anamweleza mjombake Kabitho kuwa, msichana aliyetaka kumwoa ni Mtange kumaanisha kuwa hakutambua vitisho, woga wala uhasama uliokuwepo baina ya makabila hayo mawili. Nali anamweleza babake Chebwe kuwa Wandiku si wezi kama alivyodai na badala yake anawataja kama marafiki zake. Vijana wengine kama vile Chugu na Toiche waligundua kuwa vitisho vya kikabila vilikusudiwa kuwafaidi viongozi wala sio raia wa kawaida. Hii inawafanya kushirikiana na wenzao ili kubadilisha hali.

Katika *Seserumbe,* Waziri Seserumbe mwenyewe anamwonya Kembo. Huyu ni kijana mhasibu katika wizara ya Utandawazi, Uchukuzi na Teknohama. Seserumbe anamwonya Kembo baada ya kumwamrisha aandike hundi ya Mkota hata bila kutimiza kanuni za

kandarasi kulingana na maagizo ya sheria. Vilevile anamwonya kijana huyo dhidi ya kubishana naye kila wakati anapotaka jambo la kifisadi lifanywe kwani angeumia. Hata anamwachisha kazi baada ya kumtahadharisha dhidi ya kuwachochea wafanyakazi walipodai kufanyiwa haki wizarani.

Katika mikutano ya kuomba kura za ubunge, Seserumbe anababaika baada ya Kembo kudai kuwa watoto walikwa wakiuza dawa za kulevya badala ya njugu kama alivyohadaa waziri. Anatishwa kwamba angepelekwa mahakamani na hatimaye kufungwa kifungo kirefu cha kumfaya awe anahamishwa tu jela inapopakwa rangi.( uk 88)

Seserumbe anaonekana kutishwa na werevu wa kijana mmoja kwenye umati wa watu waliokuwa wakidai haki dhidi ya nyumba zao kubomolewa. Anamdadisi Yamwaka na kutoa vitisho vya kumwangamiza kijana yule kutokana na kauli yake:

> ...Nichunguzie huyu kijana, nataka kujua yeye ni nani, anatoka wapi, anahusiana na nani, ...yaani chunguza nani, gani na nini zake zote, bila kubakiza hata moja. (uk 67)

Vijana wanaonekana kutotiwa hofu na vitisho hivyo vya waziri. Kembo hakuogopa vitisho vya Sesermbe bali aliendelea kumhimiza atende haki kwa mujibu wa kanuni za kazi. Hatimaye, bila woga Kembo anawaeleza wapiga kura kuhusu maovu yote aliyokuwa akiyatekeleza waziri Seserumbe. Kwa njia hii ya kukabiliana na Seserumbe bila kuogopa vitisho vyake anamwambia waziri kuwa uongozi ni kama ng'ombe wa kuazimwa na kama ilivyo katika jamii hiyo ng'ombe kama huyo hawezi kujazi zizi. Mwishowe, Kembo anafaulu kuwahimiza wapiga kura kumwondoa Seserumbe uongozini.

### 2.2.2 MAAMUZI MABAYA

Katika tamthilia tunazozihakiki, kuna ushahidi tosha kuwa viongozi na watu mbalimbali wenye mamlaka wanayafanya maamuzi mabaya. Maamuzi haya yanawaathiri wanajamii, hivyo kuzua migogoro inayopelekea upinzani wa kutaka mabadiliko.

Katika *Kifo Kisimani,* Bokono anafanya maamuzi mabaya kwa kutoa amri ya kupiga marufuku matumizi ya kisima na bonde la Ilangi. Haya ni maamuzi mabaya kwa sababu, Wanabutangi walinyimwa haki ya kuyapata mahitaji yao ya kimsingi. Maamuzi haya ndiyo hatimaye yanaibua hisia za upinzani unaopelekea kuporomoshwa kwa dikteta Bokono. Maamuzi mengine aliyoyafanya Bokono, ni kuamuru Mwelusi kutiwa gerezani na hatimaye kuuawa. Haya ni makosa makubwa kwani yanaashiria kutokujali wala kuthamini maisha ya raia. Makosa hayo yanazua ghadhabu za raia ambao wanajitoma katika ikulu na kumporomosha Bokono toka mamlakani.

Mwelusi aliapa kuwapigania Wanabutangi hadi warejeshewe haki zao. Anamwambia Zigu kuwa, silaha hazingetosha kuwapokonya Wanabutangi haki zao. Anafafanua kwa kusema kuwa, mpango wa utawala ulikuwa ni kuligeuza Bonde la Ilangi liwe mali ya Bokono na wenzake. Kwa hivyo, alitaka maamuzi haya mabaya yabatilishwe kupitia kwa Wanabutangi waliokuwa tayari kama anavyosema:

> ...Wanabutangi ni wengi. Watakomboa
> Kisima cha Mkomani. Watakomboa Bonde la
> Ilangi. (uk94).

Katika tamthilia ya *Seserumbe,* waziri Seserumbe anafanya maamuzi mabaya. Hii inafanyika anapochukua pesa zote zilizokuwa zimekadiriwa kuwalipa wafanyikazi walioomba malipo

awali kutimiza dharura zao. Wafanya kazi wanapogundua tabia hii wanalalamika kwa kufanya maandamano ambayo yanafungua mwanya wa kuchunguzwa kwake.

Pia waziri anafanya makosa ya kulangua mihadarati na kuwatumia watoto katika biashara yake haramu. Anawahadaa raia kuwa, watoto wao walikuwa wakiuza unga na njugu. Ukweli hatimaye unajulikana baada ya madawa hayo kuanza kuwaharibu vijana akili. Ni kwa sababu hii ambapo wazazi, ambao ni wapiga kura wanaamua kutomchagua kama mbunge. Anapopoteza kiti cha ubunge wake, hapo nafasi ya kuteuliwa kama waziri inapotea pia.

Vilevile, waziri Seserumbe anafanya makosa mabaya ya kukiuka kanuni zilizowekwa kuhusu malipo ya kandarasi. Anapotoa uamuzi kuwa Mkota aandikiwe hundi bila kukaguliwa na kuidhinishiwa miradi aliyopewa, waziri alikuwa anajitia katika kashfa iliyomletea matatizo baada ya wakaguzi wa hesabu kugundua matumizi mabaya ya pesa za wizara.

Kembo, mhasibu mkuu katika wizara alikuwa akimtahadharisha dhidi ya kufanya maamuzi mabaya na mambo kinyume cha kanuni. Alikuwa amemdokezea kuwa pangekuwa na tatizo baada ya yeye kuamua kuzichukuwa pesa zote zilizopangiwa kupewa wafanya kazi kwa maombi ya kushughulikia dharura zao na kuwalipa vibarua. Pia anamtahadharisha kuhusu maamuzi yake ya kukiuza kipande cha ardhi kilichopangiwa upanuzi wa barabara. Kembo anamwonya kuwa jambo hili lilikuwa hatari kwa vile hiyo ilikuwa ardhi ya umma iliyouziwa kampuni ya kibinafsi.

Kembo anaendelea kuwatetea watu wa eneobunge la Madongoporomoka alilokuwa akiliwakilisha Seserumbe. Hii ilihusu makazi yao duni yaliyokabiliwa na hatari ya kubomolewa ili barabara ijengwe mahali hapo. Anamfahamisha Seserumbe kuwa alikuwa

akijitia kwenye jiriwa ambalo lingemwangamiza. Hili linajitokeza hatimaye tunapowaona wanaeneobunge lake wakimkemea kama kiongozi asiyewajali.

Tamthilia ya *Maua Kwenye Jua la Asubuhi,* Chebwe, Kabitho na Tungai wanafanya maamuzi mabaya. Maamuzi yao ya kushiriki katika vita ndiyo yaliyosababisha vifo na mateso ya watu kutoka makabila ya Wandiku na Watange.

Chebwe ni kiongozi wa Watange, na kwa ufadhili wa kuwannunulia zana na kufanya mipango mingineo, anakuwa mbabe wa kivita asiyethamini maisha ya binadamu.

Kabitho naye ni mfadhili wa vita upande wa Wandiku. Anakubali kuchochewa na wanawake wanaomwambia kuwa, hapakuwa na mwanamume aliyebaki katika kabila la Wandiku na hivyo, alifaa kuvaa rinda kama wanawake wenzake. Ghadhabu yake inamsukuma kumlipa Tungai, mwanajeshi aliyestaafu ili awafunze vijana vita vya kukabiliana na Watange. Hayo yalikuwa maamuzi mabaya kwa sababu yangesababisha mauaji ya halaiki iwopo vita vingezuka.

Tungai pia alifanya maamuzi mabaya baada ya kupuliziwa sumu ya uchochezi wa Kabitho. Kama mwanajeshi alijua fika kwamba, vita vya kikabila ni kitendo cha uvunjaji sheria. Matokeo ya kuwafunza vijana mbinu za vita yangekuwa makosa yaliyovunja mkataba wa 'Geneva' kama mwenyewe anavyosema.

Vijana wanagundua njama za matayarisho na mipango ya maababe wa vita. Wanajadili hatua ambazo wangelizichukua ili kuepusha janga la vita lililoziikabili jamii zao. Chugu, kijana mwanafunzi, anawaelezea Waito na Nali alivyokuwa ameingizwa kwenye mipango ya vita. Yeye pamoja na vijana wengine walikuwa wafunzwe kupigana kwa niaba ya Wandiku ili

kuwashambulia Watange iwapo wangewashambulia. Anawatambua Kabitho kama mfadhili na Tungai kama anayetoa mafunzo ya kivita.

Hapo hapo, Chugu anawafahamisha wenzake kuwa babake Nali, alikuwa akishiriki katika mpango kama huo wa kivita kwa upande wa Watange. Waito anaongezea uzito kwa kuwafahamisha kuwa rafiki yake Mtange kwa jina Toiche, alikuwa akiinunua mishale sokoni katika kibarua alichopewa na Chebwe.

Vijana hawa wanafanya uamuzi wao ili kukabiliana na mipango hii ya wazee wao. Waito anamnasihi mjombake kutafuta njia badalia na kuepuka vita. Naye Nali anaahidi kumshinikiza babake kuacha hujuma alizokuwa akiwapangia Wandiku.

Kitu kinachowasukuma vijana hawa kujitahidi kuwabadilisha mawazo wazee wao ni maafa walioyashuhudia walipoenda ziara Lipodia na sehemu nyinginezo barani Afrika kama anavyosema Waito:

> ...ewe Afrika na rangaito zako za damu...niliwaona viguru kadha, kazi ya mabomu ya kutega. Matokeo ya uhasama katika jamii. Matokeo ya kutoelewana na kutovumiliana...(uk 57).

Waito akikabiliana na Kabitho na Tungai, anawaambia kuwa moyo wake ulikuwa unawashawishi waache kuingia vitani. Anawanasihi huku akisema kuwa, japo umri wake ni mdogo, wayatilie maanani mawaidha yake. Anawapendekezea njia badalia za kukabiliana na uhasama baina yao na watu wa kabila la Watange. Pendekezo lake ni kuwa watumie vyombo vya serikali, mahakama za kimataifa na hata maandamano ya kila siku ya kupinga mipango ya vita.

Nali anakabiliana na babake Chebwe na kumhimiza atambue kwamba hata Wandiku walikuwa na utajiri wa kuwawezesha kuzinunua silaha kali. Ushindani huu wa ununuzi wa silaha ni hali ambayo ingelifanya kila kabila kujihami kwa zana hatari zaidi.

Kuhusu mizozo ya ardhi, Nali anamweleza babake kuwa hili lilikuwa swala gumu. Anamfahamisha kuwa hata Wandiku aliodai wameichukuwa ardhi ya Watange, walikuwa na matatizo yao. Kwa hivyo, kulingana na Nali hili ni swala linalofaa kutazamwa kwa undani anaposema:

> ...Kuna matatizo ya kimsingi kuhusu ardhi katika nchi.
> Watu wachache wana ekari maelfu wakati watu wengine
> hawana hata futi kumi mraba za udongo...Kuna matatizo ya
> ardhi yanayohitaji kutatuliwa ...kwa kutumia sheria na sera
> sio mishale na mikuki.(uk 60-61).

Tunaona juhudi za vijana hawa zikizofanikiwa kwani wazee wao wanaonekana kulegeza misimamo yao mikali. Tungai anatudokezea uwezekano wa Chebwe na Watange wenzake kushiriki katika juhudi za kutafuta suluhisho la mizozo yao kwa njia ya amani badala ya kupigana.

### 2.2.3 KUTOZINGATIWA MAADILI

Katika *Seserumbe,* Waziri Seserumbe hazingatii maadili ya kazi. Kutowajibika huku kunajidhihirisha anapomwamrisha Kembo kuandika hundi ya malipo kwa bwana Mkota. Maadili ya kazini yalihitaji wakaguzi kutoa ripoti ya kuonyesha kuwa mwanakandarasi alikuwa amefanya kazi kikamilifu.

Waziri Seserumbe pia anakosa maadili anapojiingiza katika ulanguzi wa dawa za kulevya na kuwatumia vijana na watoto wa Madongoporomoka kuzieneza mahali kwingi kama vile anavyosema mwenyewe anapoingiwa na kiwewe:

> ...watoto wauza njugu, wanauza njugu ***kila mahali***! Wauza njugu ***mijini***! Wauza njugu katika ***mitaa ya mabanda***! wauza njugu ***barabarani***!...kwenye ***viwanja vya michezo!....shule za nchini***! Wauza njugu ***kila mahali***(uk 54. msisitizo ni wetu.)

Huu ni ukosefu wa maadili kwa sababu dawa za kulevya ni janga linalowafanya vijana hao kuharibika akili. Ni kosa kubwa zaidi ikizingatiwa kuwa anayeiendesha biashara hii haramu ni waziri anayehudumu katika serikali inayotawala Monipeyi.
Kembo anajiwajibisha na kuwaeleza wapiga kura ukweli kuwa, watoto hao walikuwa wakiuza dawa badala ya unga na njugu kama alivyowahadaa waziri.

Maadili ya uchaguzi pia hayakuzingatiwa katika nchi hii. Waziri Seserumbe anaungama kosa hili anaposema wazi kuwa, alishinda hata baada ya kuchaguliwa na watu wachache. Ushindi kutokana na kuchaguliwa na watu wachache ni kinaya kikubwa. Kembo anapofanya kampeni yake na kuwafahamisha watu ukweli anafaulu kuzoa kura zote na kuhakikisha kuwa Seserumbe hakuwa na mwanya wa udanganyifu.

Seserumbe vilevile anaonyesha ukiukaji wa maadili anapojiingiza katika uhusiano wa kimapenzi na Belinda, mhazili wake wizarani. Ni wazi kuwa Belinda amekuwa katika uhusiano huu wa nje ya ndoa kwa muda mrefu, na hata nyumba walikokuwa wakiishi na

mumewe ilikuwa ya Seserumbe. Wafinyakazi wanapougundua uhusiano huu, wanamchagua Maribel badala ya Belinda ili kuhakikisha kuwa siri zao hazimfikii waziri.

Seserumbe anamfuta bintiye kazi baada ya kugundua kwamba alikuwa amechaguliwa kama mwakilishi wa vijana katika chama cha wafanikazi wa wizara. Hiki kilikuwa kitendo cha ukiukaji maadili kwani alitaka kumlazimisha Maribel kujinyenyekesha kama binti badala ya mwajiriwa wa kawaida katika wizara. Baadaye tunafahamishwa kuwa alimfuta Maribel kazi kutokana na sifa zake za ushawishi mkubwa katika chama cha wafanya kazi waliokuwa wakidai haki zao wizarani.

Katika *Kifo Kisimani,* Bokono amefanya mambo mengi ya ukosefu wa maadili ya kiutawala. Kwa ujumla, tunaweza kusema kuwa, kwa muda mrefu, hapakuwepo na uchaguzi wowote Butangi. Ni wazi pia Bokono hakuwa na mpango wowote wa kufanya uchaguzi kwa vile alijiratibia kuongoza Butangi kwa miaka mia moja. Bokono vilevile anakiuka maadili katika mahusiano ya mamlaka anapodai hakuchaguliwa na Wanabutangi bali aliketishwa kwenye kiti cha enzi na Mungu. Kauli hii anaitumia ili kujipa liseni ya kutowawajibikia Wanabutangi ambao kulingana naye, hawakumchagua na hakutarajia kupingwa na yeyote. Anakuwa ni dikteta mwenye nguvu nyingi kupindukia hasa tukitilia maanani kuwa washauri wake walimhakikishia kuwa angeongoza kwa miaka mia.

Kupitia maneno ya Kaloo tunautambua ukosefu mwingine wa maadili wa Bokono. Katika kisa hicho, Bokono alikuwa amefumaniwa na mkewe Nyalwe akiwa na hawara katika tendo la ngono.

Kifo cha Mwelusi kinakuwa ni kichocheo kikuu cha kuuondolea mbali utawala usiofuata maadili. Kulingana na Atega, baraza la hukumu lingebuniwa ili kuhakikisha kuwa hukumu za haki zimetolewa ili kuendeleza uongozi wenye kuzingatia maadili.

Washauri wa Bokono wanakosa maadili katika kazi zao. Hii ni kwa sababu hawakutoa ushauri ambao ungechangia uongozi mzuri na wenye kuridhisha. Batu na Zigu wanadhihirisha ubinafsi na ukatili katika matendo yao.

Mwelusi anapokabiliana nao anawaeleza kuwa uzalendo halisi unafaa kuwa ule wa kuipenda Butangi bali si Bokono. Batu anapomwacha awazie kuhusu kujitangaza kama mchochezi anamjibu kwa kusema kuwa:

> Natumiwa na fahamu zangu ili kuiboresha Butangi...
>
> Butangi ni kubwa kuliko utawala wa Mtemi yeyote.
>
> (uk 33)

Katika *Pango,* Ngwese hana maadili katika utunzaji wa hazina ya umma. Anashirikiana na wakoloni ili kulipora pango. Vilevile tunafahamu kuwa, alipokuwa katika shirika la umma alishiriki katika kashfa ya matumizi mabaya ya fedha. Kwa hivyo, ni wazi kuwa hakuzingatia maadili katika utekelezaji wa majukumu aliyopewa.

Maadili ya uchaguzi vilevile hayakufuatwa nchini Chemwa. Ngwese alimshambulia mpinzani wake na kuwahonga wapiga kura kwa kuwapa machungwa. Hii inamaanisha uchaguzi wenyewe ulikuwa si wa kweli na haki kwani ulikumbwa na udanganyifu. ( Uk 47).

Katika kukabiliana na maovu haya, Katango anawahimiza vijana na wapiga kura wengine kupuuza vishawishi vya Ngwese. Pale wanapopokea machungwa na kubadili nia ya kumchagua anaulalamikia usaliti wao akisema:

> I wapi dhamiri tuliyoikazania?
>
> I wapi nia tuliyoishikilia?
>
> I wapi historia tuliyoijua?
>
> Sote tulikubaliana ...(uk 49)

Hata hivyo, hakufa moyo kwani anaapa kuwa, hataacha kulistahi pango hata pale atakapohitimu ndoto yake ya kuliongoza pango. Anaelewa kuwa ushindi wa Ngwese ulikuwa wa uongo. Anaonya kuwa ushindi wa aina hiyo huwa haudumu kwa muda mrefu anaposema kuwa:

> ...ndoto yangu na kizazi changu siachi...huo ni
> ushindi wa uongo...una miguu mifupi (uk. 49).

Katika *Maua Kwenye Jua la Asubuhi,* Chebwe, Kabitho na Tungai hawakuzingatia maadili yanayomwajibikia kila mwanajamii kuwa na moyo wa kumjali mwenzake na kuzuia umwagikaji wa damu.

Chebwe anafadhili vita upande wa Watange naye Kabitho upande wa Wandiku. Hawa wawili ni viongozi wanafiki wanaolenga kuyatumia makabila yao kupigana ili wafaidi wenyewe. Chebwe alitamani kuwa waziri katika serikali mpya naye Kabitho hakutaka kuyapoteza mashamba yake makubwa yaliyopandwa ngano.

Chebwe alikosa maadili kwa kufanya matendo yanayokiuka kanuni za uchaguzi. Mpango wake ulikuwa kwamba, uchaguzi unapokaribia, wageni wote katika eneo lake la uwakilishi wafukuzwe na wengine wauawe ili wasipige kura za kumpinga. Aliandama ndoto yake ya kuwa waziri serikalini kwa njia yoyote ile hata kama ingehusisha umwagikaji wa damu.

Tungai na Toiche wanafanya makosa ya kutayarisha vita na kuwalisha vijana viapo. Walitumia propaganda ya kuwahadaa kuwa walikuwa wanashiriki vita vya kukomboa kabila lao. Tungai alikuwa na makosa makubwa kwa vile alipokuwa katika jeshi alifahamu kanuni na sheria zinazofaa kuwekwa kudhibiti vita kwa mujibu wa maazimio ya Geneva.

Maamuzi yao mabaya yanapojulikana na vijana, yanapingwa vikali. Waito, Nali na Chugu wanajuzana kuhusu walichokijua kuhusiana na maandalizi ya vita. Chugu anawafahamisha kuwa wafadhili wa vita pande zote mbili walikuwa Kabitho na Chebwe. Pia wanafahamishana kuhusu mchango wa Tungai kama mfunzaji wa wapiganaji Wandiku naye Toiche kama aliyekuwa akiikusanya mishale.

Wanayatumia maarifa yao pamoja na tajriba waliokwishaiona katika maeneo yaliyokuwa na vita vya kikabila. Kila mmoja wao anawahimiza watu wa kabila lake kuepuka vita na kutumia njia nyingine badala ya vita. Mwishowe, tunaarifiwa na Tungai kuwa, palikuwa na uvumi kwamba Chebwe na kundi lake, walikuwa tayari kutafuta suluhu ya migogoro yao kwa njia ya amani.

## 2.3 MAOVU YA KIUCHUMI

### 2.3.0 UTANGULIZI

Maovu ya kiuchumi tunayoyachanganua katika sehemu hii yanahusiana na ufisadi. Haya ni pamoja na matumizi mabaya ya mali au raslimali za umma, matumizi ya cheo au nafasi ili kujinufaisha kibinafsi, kujipatia pato lisilo halali, wizi wa mali ya umma, kujilimbikizia mali, ubadhirifu na matendo yoyote yale yanayopuuza maadili ya kiuchumi.

Kulingana na Foucault (1982), Maadili katika mahusiano ya mamlaka hutarajia umma kuhusishwa na kile wanachokizalisha. Ukosefu wa uzingativu wa kaida hii, huzalisha upinzani kutoka kwa watawaliwa. Hii huwa ni katika jitihada zao za kujirudishia uwezo wa kudhibiti mali na raslimali zao.

Ufisadi kuligana na Sercombe, (1997) ni hali ya kutumia mali ya umma kwa kujifaidi kibinafsi, bila ya kuwapa nafasi waliozalisha mali hayo kufaidi.

Katika sehemu ifuatayo, tunaangazia sura mbalimbali za ufisadi unaopatikana katika tamthilia nne tulizoziteua. Ufisadi huu unatekelezwa na watu wa ngazi, matabaka na vyeo mbalimbali. Ijapokuwa ufisadi wa kiwango cha juu unaendeshwa na viongozi, kunao ushahidi wa kuonyesha kuwa wanaotawaliwa hujihusisha katika maovu mbalimbali ya kiuchumi katika mahusiano yao ya kila siku.

**2.3.1 UFISADI**

Ufisadi ni maovu ya kiuchumi yanayohusu uharibifu na matumizi mabaya ya mali ya umma, cheo au nafasi aliyonayo mtu. Katika tamthilia tunazozihakiki, tumeeangazia matumizi mabaya ya mali ya umma, uhongaji, ubinafsishaji wa raslimali za umma, ujilimbikiziaji, uporaji na wizi.

Katika tamthilia ya *Pango,* jamii ya Wachemwa inapomteua Ngwese kuwa mlinzi wa pango, walitarajia angewatunzia hazina inayowakilishwa kistiari na asali. Badala ya Ngwese kutekeleza matumizi yafaayo ya asali hii, anashirikiana na Wachemwa wachache pamoja na wakoloni wa nchi hiyo, kupora na kuitumia asali hiyo kwa manufaa yao wenyewe.( uk 75)

Ngwese pia anahusishwa na ufisadi alipokuwa katika shirika moja la umma. Mwishoni mwa tamthilia tunawaona askari wawili waliomtia mbaroni kwa tuhuma kwamba, alikuwa amefuja mali ya umma alipokuwa mkurugenzi wa shirika. Ngwese katika uzungumzi nafsia, anakiri kuwa ushahidi wa ufisadi huu ulikwishafutiliwa mbali kwa kuwatumia makachero marafiki zake (uk 51).

Ufisadi mwingine unajitokeza pale ambapo Ngwese anatumia vishawishi wakati wa uchaguzi ili kubadili nia za wapiga kura. Anatumia machungwa ambayo ni sitiari ya hongo. Ngwese anapokitumia cheo chake kumtafutia Kauleni kiwanja cha kujengea hoteli na leseni ya kuendesha biashara yake, ni ufisadi. Anaendelea zaidi pale anapomshinikiza Kauleni kumuunga mkono kutokana na mchango wake wa awali.

Katango pamoja na vijana wenzake wanayaangazia matendo ya Ngwese ili kuwadhihirishia Wachemwa ukweli kuhusu kiongozi wao. Katango anaendelea kuwaeleza watu kuwa, si yeye wala watoto wao waliocheza pangoni kama alivyodai Seki na Ngwese. Anawafahamisha watu kuwa, waliokuwa wakicheza pangoni walikuwa malaghai waliokusudia kuipora asali.

Katango, Kibwana na Kikubi wanafuatilia kwa makini yanayooendelea pangoni. Ngwese akishirikiana na wengine, wanamtia Katango kitata kwa uganga ili asiweze kuwafahamisha watu ukweli kuhusu aliyekuwa akicheza pangoni. Susa na Sota wanajionea watu waliokuwa wakizungumza kwa kidhembe huku wakijinata kuwa wataila asali yote bila kubakisha chochote. Katika kisa kingine Susa na Sota wanashuhudia watu watano wakicheza kwenye lango la pango. Mkuu wao alikuwa akijinata na kupanga vile ataiuza asali na kujipatia fedha kama vile dola, pauni, yuro na yeni. Hii ilikuwa sauti ya Ngwese aliyekuwa akishirikiana na wakoloni wanaowakilishwa na sarafu za pesa kutoka nchi zao yaani, Dola ya Wamarekani, Yuro ya Yuropa, Pauni ya Uingereza na Yeni ya Ujapani. Haya yote ni mataifa yanayotumia utandawazi kama wizi wa kuzipora raslimali kutoka mataifa ambayo hayajaendelea au kubaki nyuma kama Chemwa. Majitu yanapokutana pangoni, Ngwese ambaye ni Jitu I, anayaahidi majitu mengine kuwa yeye ni mrija na angefyonza kila kitu ili wakihamishe na kukipeleka ughaibuni.

Katango licha ya kitata alichotiwa, anawaongoza vijana wenzake na Wachemwa wengine ili kushuhudia wizi wa asali pangoni ulioongozwa na Ngwese. Wanapoyavua majitu maguo yaliyokuwa yamejivika nyusoni, wanagundua kuwa walikuwa ni akina Ngwese na wezi wenzake. Hapa kila mtu anakubali kuwa Katango alikuwa akiwajuza ukweli.

Kwa juhudi hizo za Katango na vijana wenzake, Ngwese anatiwa pingu na kupelekwa mikononi mwa sheria ili kujibu mashtaka. Jambo hili lilichangia kuleta mabadiliko kwani Katango alipewa mamlaka ya kuliongoza pango. Kutokana na sifa tunazozijua kuhusu Katango, lazima pango lingeongozwa kwa uadilifu wenye kuwanufaisha na kuwafurahisha Wachemwa wote.

Katika *Kifo Kisimani,* Bokono anawaongoza wafisadi wengine. Kwanza anabinafsisha Bonde la Ilangi na pia kuweka marufuku ili Wanabutangi wasikitumie kisima cha Mkomani kwa siku nne katika juma.

Bokono vilevile anaunga mkono ufisadi unaoendelezwa katika idara mbalimbali za Butangi. Bokono anatetea kitendo cha unyakuzi wa uwanja wa kuchezewa na watoto. Hii ilitokea baada ya uwanja huo kupewa mkuu wa askari ili kumfanya amtii Bokono na kuendelea kuwatia raia woga.

Bokono vilevile ni fisadi kwa vile anatumia mahusiano ya kifamilia na upendeleo katika uajiri. Mmoja wa washauri wake Kame, ameajiriwa kwa kuwa kakake Nyalwe. Vilevile tunafahamishwa kuhusu mtoto wa Kaloo aliyeajiriwa kwa sababu Bokono alimpendekeza.

Mkuu wa washauri wa Bokono Batu, anauendeleza ufisadi pale anapomwahidi Mwelusi utajiri mkubwa. Mwelusi alitakiwa kukiri na kutangaza hadharani kuwa amejitenga na kundi

haramu la Kabakaba. Kutokana na hayo, angepewa ardhi, mifugo na cheo cha kuwa kiongozi wa vijana . Ni wazi kuwa Mwelusi hakuyastahili malipo kama hayo. Vishawishi hivi ni ishara ya ufisadi wanaouendeleza washauri wa Bokono ili kuuzima upinzani wowote. Kwa hakika haya ni ya umma ambayo yangetumika kwa njia isiyofaa.

Makachero Mweke na Talui vilevile wanachangia ufisadi wanapomwidhinisha Gege kutunukiwa Mkuki wa Almasi huku tukijua kwamba, kazi aliyoifanya haikustahili kufidiwa kwa tunu kama hiyo.

Mwelusi katika tamthilia hii anakuwa ni kichocheo kikubwa katika kubadilisha hali mbaya iliyokuwepo. Anaupinga utawala wa Bokono dhidi ya ufisadi wa kubinafsisha Bonde la Ilangi na kukitumia Kisima cha Mkomani peke yake kwa siku nne katika juma. Mwelusi anamfahamisha kakake Gege kwamba, palikuwepo na uvurugaji wa kanuni tangu enzi za Mtemi Mrima.

Mwelusi akishirikiana na Atega, pamoja na wazalendo wengine wanahakikisha kuwa Bokono ameondolewa madarakani. Kifo cha Mwelusi kinakuwa ni kafara ya kuitakasa nchi ya Butangi.

Katika tamthilia ya *Seserumbe,* Waziri wa Utandawazi, Uchukuzi na Teknohama anatumia pesa katika wizara hiyo kifisadi. Njia ya kwanza ya kufisidi wizara ni katika kumlazimisha mhasibu wake Kembo kuvunja mipango na taratibu za malipo pale wizarani. Analazimisha kulipwa pesa nyingi za burudani na maslufu mengine badala ya kuwalipa vibarua na waliokuwa wameomba malipo awali ya dharura.

Njia ya pili ni katika kumshurutisha Kembo kumwandikia Mkota hundi bila kufuata kanuni za serikali. Mkota ni mwanakandarasi katika kampuni ya ujenzi ya *Acme.* Mara kwa mara walishirikiana na waziri katika kuifisidi wizara kwa kughushi au kukiuka kanuni za utoaji

huduma. Seserumbe alikuwa akiitetea kampuni ya *Acme* iliyomilikiwa na Mkota ili ipewe kazi wizarani. Hatimaye, wawili hao walikuwa wakigawana mapato hayo kimafungu.

Seserumbe alipokuwa akimsaidia Mkota kulipwa, alidai kuwa hata Meya na madiwani wengine walikuwa na kashfa. Kwa kuzijua kashfa za wengine, Seserumbe anataka kuhalalisha ufisadi wake. Mpango wake ulikuwa kwamba atawatisha wahusika katika kashfa hizo na kuwashinikiza hadi wayaidhinishe malipo hata bila ya kuzingatia kanuni za utendakazi.

Kembo anakabiliana na waziri na kumfahamisha kuwa malipo hayangetolewa bila ripoti ya wakaguzi. Hawa walihitajika kuthibitisha kuwa kazi ilikuwa imekamilishwa kwa kuzingatia viwango tarajiwa. Waziri anapokazania kuwa lazima hundi iandikwe, Kembo anamtaka kuandike barua kuonyesha kuwa aliidhinisha malipo yasiyofuata kanuni. Haya yote yanaonyesha kuwa Kembo alitaka kuwepo na mabadiliko katika utendaji kazi wizarani.

Kembo pia anaonyesha wafanyikazi wa daraja za juu kama wafisadi kwa kuidhinisha kuongezewa mishahara yao mara tatu huku wale wa daraja za chini wakibaki bila nyongeza kwa miaka minne. Kembo anaufichua ufisadi zaidi anaposema kuwa, wafanyikazi wakuu walikuwa wakighushi stakabadhi za malipo ya usafiri walipotoka kwenye sehemu zao za kazi anaposema kuwa:

> …mameneja wanaposafiri nyanjani au kwenye warsha zao wanarejea na stakabadhi za *dinner* moja ya shilingi thelathini elfu, hata wanapokwenda maeneo ambayo hayana hoteli isipokuwa vijihoteli… (uk. 30).

Kijana mwingine anayepigania mabadiliko wizarani ni Maribel bintiye Seserumbe. Yeye kama mwakilishi wa vijana katika chama cha wafanyikazi wizarani anaungana na wenzake katika kudai malipo na huduma bora kazini.

Kembo vilevile hachoki katika kumkumbusha waziri Seserumbe kuhusu kashfa alizozishiriki. Katika kashfa mojawapo, Seserumbe alihusika kwenye unyakuzi wa uwanja uliotengewa upanuzi wa barabara. Uwanja huu uliuziwa Machina waliojenga kiwanda cha usindikaji wa mafuta. Seserumbe alikuwa amenufaika kutokana na mauzo ya ardhi hiyo. Hii ndiyo sababu anadai kuwa, barabara inajengwa katika eneo la makazi duni. Anapojulishwa kuwa kanuni za uuzaji ardhi ya umma hazikuzingatiwa anasema:

> …umma gani? Umesikia wapi
> umma unamiliki ardhi wewe? (uk 47)

Kembo kwa upande wake hachoki kumkumbusha Seserumbe kuwa, ardhi ya serikali haifai kuuzwa kwa njia alizofuata yeye. Kadhalika anaonyesha kuwa, watu kutoka eneobunge lake walikuwa hawakuridhishwa na ufisadi wenyewe anapomwambia:

> …na hawa waliokuchagua…uliazimwa ng'ombe wa wenyewe nawe ukammiliki…umemkamua mpaka kiwele kimekauka maziwa nawe kama kupe unang'ang'ania kwenye ngozi…ukasahau… ng'ombe hakamuliwi maziwa mchana (uk.90).

Ghadhabu ya wapiga kura, inawapelekea kumchagua Kembo kama mwakilishi wao kwa vile aliwatetea walipobomolewa mabanda yao.

Aina nyingine ya ufisadi ni pamoja na ubadhirifu. Huu ni utumizi wa mali kwa njia isiyofaa au inayokiuka mipaka.

Tunashuhudia katika *Kifo Kisimani,* vishawisi vya dhamana kubwa kupindukia vikitumika ili kuwamotisha watu kutekeleza mambo mbalimbali. Gege anaahidiwa mali mengi iwapo angekubali kumsaliti na kumuua kakake Mwelusi. Hapa ubadhirifu anajitokeza upande wa utawala ambapo watu wasiostahili tunu wanatunukiwa kwa kufanya mambo maovu.

Mwelusi anaahidiwa utajiri mkubwa sana iwapo angetangaza hadharani kuwa alikuwa ameuasi uchochezi. Ukweli hapa ni kuwa utawala wa Bokono ulikuwa tayari kutumia utajiri mkubwa wa kitaifa katika kufanya mambo yasiyo halali. Huu ni ubadhirifu. Kwa Mwelusi, vishawishi hivi havikuwa na maana kwani yeye alitamani kuona mabadiliko yenye kumfaidi kila Mwanabutangi.

Seserumbe anapodai alipwe takrima mara dufu anaudhihirisha ubadhirifu wake wa kutaka kupewa pesa zote walizokuwa walipwe wafanyikazi wengine vibarua na mahitaji ya dharura waliyokuwa wameomba awali. Kembo anamnasihi atupilie mbali wazo lake la kuzoa pesa zote. Badala yake anampendekezea awe na subira hadi juma lililofuata ili atayarishiwe malipo hayo ya takrima.

Bado katika wizara, palikuwepo na ubadhirifu uliowahusu wafanyikazi wa daraja za juu. Hawa walidai pesa nyingi kupindukia waliposafiri nje ya sehemu zao za kazi. Kwa mfano, kunao mameneja waliodai kulipiwa chakula cha jioni-*dinner*, ya shilingi elfu thelathini hata pale ambapo hapakuwa na mikahawa ya kuuza vyakula ghali jinsi hiyo.
Kembo katika kuitetea posho ya wafanyakazi wa viwago vya chini, anahimiza kuwa hata wao walifaa kushughulikiwa badaala ya marupurupu yao kupunguzwa kama ilivyokuwa imefanyika.

### 2.3.2 ULANGUZI

Ulanguzi ni uendeshaji wa biashara haramu yenye kuwadhuru watu.

Katika tamthilia ya *Seserumbe* ulanguzi unajitokeza. Waziri mwenyewe ni mlanguzi wa dawa za kulevya. Ulanguzi wake ni wa kiwango cha juu sana kwani anaongea kuhusu shehena kubwa iliyopakiwa kwenye *MV Morning Glory*. Katika ulanguzi wake wa mihadarati, Seserumbe anawatumia vijana kuuza dawa hizo katika sehemu yingi. Tunamwona akitumia mikakati katika kulangua dawa hizi kama vile kuzitaja kibandia na kuziita unga au njugu karanga. Athari za ulanguzi wa dawa hizi unadhihirika wazi pale tunapowaona vijana wakiharibika akili baada ya kuzibugia dawa zenyewe.

Mhasibu wa wizara na mpinzani wa Seserumbe, Kembo, ndiye anayewafahamisha wapiga kura kuhusu kashfa hii. Anawaeleza kuwa, watoto hawakuwa wakiuza njugu kama alivyodai Sesermbe bali walikuwa wakisambaza dawa za kulevya. Anawaonyesha ukweli wa madai yake kutokana na watoto wenyewe kuharibika vichwa. Kembo anatumia maovu haya kuwahimiza wapiga kura kutomchagua Seserumbe kwani hakuyajali maslahi ya watoto wao. Biashara hii yake haramu ndiyo inayomfanya kupoteza kiti chake cha ubunge na kumsambaratisha hadi kushikwa na kichaa. Hakuamini kuwa alikuwa ametolewa madarakani na kwa hivyo anaendelea kuishi kindoto au kilevilevi kama aliyetumia dawa hizo alizokuwa akilangua.

## 2.4 MAOVU YA KIJAMII

### 2.4.0 UTANGULIZI

Maovu ya kijamii tunayoyajadili ni yale yanayohusiana na maadili. Jamii tunazokumbana nazo katika tamthilia nne tulizoziteua, zinatangamana kwa kuongozwa na maadili fulani ya kimsingi. Maadili haya yanapovunjwa, husababisha maovu ya kijamii. Mifano ya maovu tutakayoyajadili ni : chuki za kikabila, kukiukwa haki za kibinadamu, mauaji, dhuluma za aina mbalimbali, usaliti, unafiki na urongo.

### 2.4.1 CHUKI NA VITA VYA KIKABILA

Katika tamthilia ya *Maua Kwenye Jua la Asubuhi,* kuna chuki baina ya makabila ya Wandiku na Watange. Chuki hii inazalisha uhasama unaoishia kwenye vita vya kikabila. Katika vita hivi, tunashuhudia maafa na hasara baada ya mali kuteketezwa.

Uchochezi ndio unaoeneza chuki hii. Kabitho na Tungai wanaamini kuwa Watange ni maadui wanaofaa kupigwa vita. Wanawake wa Kindiku wanawachochea wanaumme katika kabila hilo. Kwa mfano Nyagathi na Gachono wanamchochea Kabitho kwa kumbeza walipomwambia:

> ...tulifukuzwa mashambani mwetu na waume wenzenu...wewe ni mwanamke mwenzetu...la hamtachukua hatua, mtaendelea kukunja mikia katikati ya miguu kutokana na woga. (uk.2-3).

Naye Chebwe anawafanya vijana Wa Kitange kula kiapo cha kuwaua Wandiku kwa tuhuma ya unyakuzi wa mashamba yao. Toiche, ambaye anaongoza shughuli za kuwalisha wanafunzi wapiganaji kiapo, anawaapisha kuzima uhai wa Wandiku na kuyageuza mali yao kuwa jivu.

Mauaji yaliyotekelezwa na wapiganaji walioongozwa na Chebwe, yalikuwa ya kikatili ambapo Wandiku wapatao thelathini na sita walifariki. Mauaji haya yanatokana na sumu inayopuliziwa vijana katika kiapo cha kikabila wakisema;

> ...Kuzima watu uhai...kugeuza mali yao jivu...kwa hivyo
>
> nisaidie ewe nafsi ya upanga na mishale. (uk 19)

Katika mashambulizi yanayoripotiwa katika gazeti la *Siku Mpya*, tunaarifiwa kuwa, watu walijeruhiwa na mali zao kuteketezwa. Nazo maiti za watu waliouawa zilikuwa na mishale miilini kama ile ya nungunungu. (uk 28)

Kabitho ambaye ni mfadhili wa vita kwa upande wa Wandiku. Anaonekana kueneza chuki za kikabila kwa kuwadunisha Watange. Yeye anadai kuwa Watange hawaaminiki na ni watu waliobaki nyuma kwa kutokuwa na akili. Anaendelea kumhimiza Tungai kuwa kabila hilo linafaa kufunzwa adabu. Hii ikimaanisha kupigwa vita vya silaha.

Waito na Nali wanayaweka wazi madhara ya vita. Vijana hawa wawili wanashuhudia maafa na hasara inayoweza kusababishwa na vita vya kikabila. Wanaeleza kuhusu walichokiona katika ziara zao kutoka chuo kikuu walikokuwa wakisomea. Nali anaeleza kuhusu mji wa Ranga katika Mto Gera, hapa aliziona maiti nyingi zilizotapakaa. Haya yalikuwa mauaji ya kabila la Ndarwa. (uk52).

Waito naye anaelezea kuhusu alichokishuhudia alipoenda Lipodia, katika hospitali ya kuwahudumia majeruhi wa vita. Aliwaona majeruhi wenye majeraha ya bomu za kutegwa ardhini. Pia palikuwepo na watoto vilema wenye miguu iliyokatwa au yenye vidonda vya risasi.

Kutokana na mauaji hayo na hasara waliyoiona, wanawahimiza wazee wao kusitisha mipango ya vita. Nali anakabiliana na babake Chebwe naye Waito anawabembeleza Kabitho na Tungai. Wazee hao mwanzoni hawakuonekana kutaka kuyasikiza mawaidha ya vijana lakini baadaye, inaposemekana kuwa Nali ametekwa nyara na Wandiku, fununu zinasikia kuwa Chebwe alikuwa na mpango wa kutafuta suluhisho la mizozo baina yao kwa njia ya amani.

Tungai naye anaonekana kukubaliana na vijana hao kuwa njia ya maandamano ingetumika katika kuishurutisha serikali kuingilia kati jambo hilo. Huu ulikuwa ushindi mkubwa kwa vijana kwani, walikuwa wameweza kuyabadilisha mawazo na fikra za wazee.

Wazo la ndoa kati ya Waito na Nali lilikuwa mkakati wa kudumu katika kuyaunganisha makabila hayo mawili. Tungai katika akili zake anaona kuwa njia hiyo ingeleta uhusiano wa kudumu ambao ungezuia vita kwa vile kila kabila lingehisi kuwa, walikuwa jamaa moja.

### 2.4.2 UNAFIKI NA URONGO

Unafiki ni hali ya kutokuwa mkweli au kujifanya kuwa rafiki wa mtu fulani ilhali ni adui. Urongo ni tabia ya kudanganya au kutosema ukweli. Kwa hivyo maovu haya mawili yana uhusiano mkubwa.

Katika *Kifo Kisimani,* Bokono ni kiongozi mnafiki. Mara kwa mara anawahadaa Wanabutangi kuwa anawapenda watoto. Kauli yake ni ya kinafiki kwa sababu tunawaona watoto na vijana wakidhulumiwa. Andua na mtoto wa Chendeke walikuwa wameumizwa na askari wa Bokono.

Katika *Seserumbe,* waziri anawahadaa wapiga kura kuwa anawapenda watoto kwa kuwapa kazi ya kuuza njugu na unga. Ukweli ni kuwa Seserumbe, anawatumia watoto hao kulangua mihadarati. Kembo anawafahamisha wapiga kura ukweli kuwa, watoto hao walikuwa wakiuza dawa za kulevya wala si njugu karanga kama alivyowahadaa waziri.

Urongo unajitokeza katika *Maua Kwenye jua la Asubuhi*, tunamuona Chebwe akimdanganya mkewe kuhusu alikokuwa wakati wa mashambulizi ya Wandiku. Ukweli ni kwamba Chebwe alihusika katika kununua petroli ya kuteketeza nyumba za Wandiku kama ilivyodhihirika katika gazeti la *Siku Mpya*. Urongo mwingine wa Chebwe ulihusu kabati kubwa na begi alizotumia kubebea na kuweka mishale.

Bintiye Nali pamoja na vijana wenzake wanagundua ukweli kwamba, kabati hilo lilikuwa la kuhifadhia mishale, na hapo ndipo harakati za kutafuta suluhu zilipoanza.

Urongo katika kiapo cha Watange uligunduliwa na Toiche anayeyelegeza msimamo kuhusu kushiriki katika vita dhidi ya Wandiku. Toiche alikwishagundua uongo na unafiki wa viongozi wa kabila lake ambao wanawatumia vijana kupigana ili hatimaye wafaidike.

### 2.4.3 DHULUMA

Dhuluma ni hali ya kuwafanyia watu wengine mambo yasiyo ya haki kwa kuwaonea, kuwataabisha, kuwadhakilisha na kuwatesa. Katika tamthilia tunazozihakiki, kuna dhuluma za aina mbalimbali kama tunazozijadili katika sehemu ifuatayo.

Dhuluma dhidi ya watoto katika *Seserumbe* inajitokeza vyema kupitia kwa tabia ya Seserumbe mwenyewe. Waziri huyu anawatumia watoto katika ulanguzi wa mihadarati. Anawafanya waenezaji na watumizi wakuu wa dawa za kulevya, jambo linalopelekea wao kuharibika akili. Waziri anawadharaulia mbali watoto hao akisema:

> ... vile vitoto na mararu Yanayofichua vitumbo vyao vilivyofuriana Vitumbo vilivyovimbiana kwa vimbizi vya uhitaji....Vyenye ramani za nyute usoni...(uk. 54).

Kembo anakabiliana na Seserumbe katika kampeni akitaka aeleze kile ambacho watoto walikuwa wakiuza. Hata baada ya Seserumbe kumtishia kuwa angeshtakiwa kwa kumharibia

jina, Kembo anaendelea kukazania kuwa watoto walikuwa wakiuza dawa za kulevya alipomwambia Seserumbe:

> ...utafika wakati kila mtu atajua watoto wanauza nini,...ukweli hauwezi kufichwa wala kufunikwa kwa blanketi...siri ya mtungi muulize kata.(uk.88).

Ukweli wa tahadhari hii unajulikana na wapiga kura baadaye wanapokataa kumchagua Seserumbe. Kembo anachaguliwa na kuwa mwakilishi wa eneo Bunge la Madongoporomoka. Haya yalikuwa mabadiliko makubwa kwani huyu ni kijana aliyeonyesha uwajibikaji wa hali ya juu.

Katika *Kifo Kisimani,* utawala wa Bokono unaendeleza dhuluma dhidi ya watoto. Tunawaona watoto wawili wakipigwa na askari. Wa kwanza ni Mtoto wa Chendeke aliyeng'olewa meno na askari alipokuwa ameenda kisimani. Wa pili alikuwa Andua aliyepata jeraha la usoni alipokuwa kisimani. Haya yanadhihirisha unafiki wa Bokono aliyekuwa akidai kwamba aliwapenda watoto. Kwa hakika watoto hao hawakuwa na makosa yoyote na ndiyo sababu Mwelusi na Atega wanaendelea kupambana na utawala wa Bokono.

Katika *Maua Maua Kwenye Jua la Asubuhi,* washambulizi Watange walisababisha vifo vya watoto watatu na mama mjamzito aliyekuwa karibu kujifungua kama lilivyoripoti gazeti la *Siku Mpya.* Ni wazi kuwa watoto walipitia hali ngumu kipindi hicho cha mashambulizi kama Neche anavyomwarifu, mmewe Chebwe kutoka gazetini:

> ...mtoto wake wa umri wa miaka 10 alifaulu kutoroka.
>
> Mtoto wa pili aliyekuwa mikononi mwake, alipatikana

> keshoye amelala, huku amekumbatia kifua cha marehemu mamake.(uk. 27).

Waito anamweleza Kabitho kuhusu maafa yaliyowajumuisha watoto ambao hawakuwa na hatia huko Lipodia, wengine walikuwa na majeraha ya risasi na mabomu ya kutegwa ardhini. Kwa huruma, anamhimiza Kabitho na Tungai kuacha matayarisho ya vita ili watoto wasije wakaumia kiasi hicho.

Dhuluma dhidi ya wanawake katika *Pango* inajitokeza kupitia kwa Ngwese. Huyu anamuona Katango kama mwanamke na kijana anayefaa kupashwa tohara na kutiwa nidhamu ya kupunguza ushindani katika nyanda za siasa na maingiliano ya kijamii. Anamtusi na kumdhalilisha anapomwambia:

> Naona babako ameshindwa nawe; labda anaistahi elimu yako lakini awe na elimu au la ***mwanamke ni mwanamke tu…mwanamke wewe,*** unajua nini kuhusu matendo…***unatakiwa kuolewa, utiwe adabu na mumeo*** (uk.10-14. Msisitizo ni wetu).

Hii ndiyo maana anahakikisha kuwa Katango na Kibwana wanashambuliwa na genge la majambazi waliojivika majuso ili wasijulikane.

Anaposhindwa kumdhibiti Katango kwa mashambulizi, anamfanyia uganga na kumtia kitata ili asiweze kunena tena. Hii ni kwa sababu Ngwese alijua kwamba Katango na vijana wengine walifahamu ukweli kwamba Ngwese na wenzake ndio waliokuwa wakipora utajiri kutoka pangoni.

Seki, babake Katango amejawa na taasubi za ubabedume. Anamhimiza bintiye kutompinga Ngwese kwani utamaduni ulimzuia kufanya hivyo. Anamtaharisha dhidi ya kushindana na Ngwese kwani nguvu zeke zilikuwa kubwa sana. Seki anawaona Katango na mamake kama watu wasio na thamani pale nyumbani.

Katango kwa upande wake hatishwi na maonevu hayo ya kitamaduni. Anawafahamisha kuwa, wakati umebadilika na wanawake wanafaa kupewa heshima. Alinuia kuonyesha kuwa, wanaumme hawangeweza kuuondolea mbali utawala wa Ngwese kwani walikuwa wakimfuata bila kuzua upinzani wowote.

Katika *Kifo Kisimani*, dhuluma dhidi ya wanawake inajitokeza kupitia kwa Nyalwe. Huyu hata kama ni mwanamke, alimshambulia hawara aliyemfumania kwake wakiwa na Bokono. Ushahidi tunaoupata kwa Kaloo unaonyesha kwamba hawara huyo alikuwa ameshambuliwa vibaya sana. Ukatili wa Nyalwe unaonekana wazi baada ya kumpiga na kumgeuza kuwa kama kuku aliyenyonyolewa manyoya na kunyeshewa na mvua ya damu.

Askari katika lango la gereza alikofungiwa Mwelusi, wanamtishia Andua kwa kusema kuwa, iwapo hakuondoka katika lango wangempiga na hata kumfanyia mengine. 'Mengine' hapa yanamaanisha kumnajisi kwa vile tayari askari III alikuwa anajaribu kumgusa Andua kifuani. (uk 35-36).

Kuna dhuluma za kimapenzi pale tunapokumbana na Zigu akimhimiza Kaloo kuzuru Ikulu ya Bokono kwani kama anavyodai Zigu, Bokono alikuwa ana hamu sana ya kuwa na uhusiano wa kimapenzi naye. Kaloo alikataa huku akidai kuwa aliogopa kushambuliwa na Nyalwe, kama alivyokuwa amemfanyia hawara wa Bokono.

Katika *Seserumbe,* kuna maonevu dhidi ya wanawake. Maribel anaeleza kuwa wafanyakazi wa kike walikuwa hawapandishwi vyeo kama wenzao wa kiume. Vilevile walibaguliwa na kulipwa mishahara midogo hata walipofanya kazi sawa na wanaume. (Uk 43)

Waziri pia alikuwa akiendeleza dhuluma za kimapenzi dhidi ya Belinda aliyekuwa mhazili wake. Anamlazimisha Belinda kumdanganya mumewe kuhusu mikutano ya urongo na hata nyumba walimokuwa wakiishi kwa muda mrefu. Nyumba hii tunafahamu ilikuwa mali ya Waziri wala si ya wizara kama mumewe Belinda alivyofanywa kuamini.

Dhuluma dhidi ya vijana katika *Kifo Kisimani* inadhihirika kupitia kwa Bokono anapoamuru Mwelusi aondolewe kwenye jamii kwani alikuwa kama mwiba. Mengi yanafanyika kudhihirisha ukatili wa Bokono dhidi ya kizazi hiki kilichodhubutu kupinga uongozi aliodai ulitoka kwa Mungu.

Katika *Seserumbe,* Waziri Seserumbe anaendeleza dhuluma dhidi ya vijana. Kwanza, anamdhihaki Kembo mara kwa mara kama mtu asiyeelewa mambo haraka. Mwishowe, anamfuta kazi kwa tuhuma ya kuwachochea wafanyikazi. Kuhusu uongozi, Seserumbe anadai kuwa, vijana hawawezi kuongoza kwa vile, ni waoga na hawajui mambo mengi. Anamfananisha Kembo na kijana mpiga kamsa pasipokuwa na sababu.

Waziri pia anamkataza bintiye kuwa mwakilishi wa vijana kazini. Anadai kuwa Maribel anautumia uhusiano wao kumchimba pale kazini. Mwishowe baada ya kuona kuwa Maribel hakujiuzulu kama kiongozi wa chama, anamwachisha kazi kwa kudai alikuwa mzembe. Kembo anawaeleza wapiga kura kwamba Waziri alimfuta Maribel kazi kwa kupigania haki za wafanyikazi na kupinga utowajibikaji wa Seserumbe pale wizarani.

### 2.4.4 USALITI

Katika *Kifo Kisimani,* usaliti unajitokeza kupitia kakake Mwelusi, Gege. Anamsaliti Mwelusi na hatimaye kumuua baada ya kuahidiwa kumwoa bintiye Bokono. Usaliti huu wake unadhihirisha ukosefu wa mapenzi baina ya watu wa familia moja.

Mwelusi anajitahidi kubadilisha mtazamo wa kakake kuhusu maisha. Anajaribu kumwonyesha haja ya kushiriki katika siasa zenye kuwanufaisha wanajamii badala ya kuandama maslahi ya kibinafsi.

Katika *Pango,* usaliti unajitokeza wakati wa kampeni. Wafuasi wa Katango, walimsaliti baada ya kupewa hongo na Ngwese. Usaliti mwingine unamhusu Ngwese, ambaye badala ya kuwajibika kama kiongozi, anajiingiza katika kashfa ya kuipora asali pangoni. Katango anafanya juu chini kuona kwamba Ngwese ametambulika kama msaliti pale alipowaongoza Wachemwa kushuhudia yeye na wenzake wakijitayarisha kuirina asali bila idhini ya raia.

### 2.4.5 UKARAGOSI

Ukaragosi ni hali ya kujidunisha kwa kumtumikia mtu kama kwamba mhusika hana akili za kujiamulia. Ukaragosi unajumuishwa miongoni mwa maovu kwa vile mara nyingi vikaragosi hawa huwa ni wasaliti wa umma unaoteseka. Vilevile hali hii ni ya kujishushia hadhi hadi kiwango cha kujionyesha kama mtu asiyeweza kutumia akili na razini inayomfanya kuwa mtu huru bali si mnyama.

Katika *Kifo Kisimani,* tunawatambua Batu na Zigu washauri wa Bokono kama vikaragosi wanaomwabudu dikteta huyo bila kudadisi au kutumia akili zao. Wanaendeleza mikakati yake na kutoa ushauri utakaomfurahisha bila kujali iwapo Wanabutangi wanaumia au la. Kwa kauli za Batu na Zigu, Bokono ataongoza Butangi miaka mia, huu ni ukaragosi wa kiwango cha juu kabisa.

Askari II na III katika gereza alimofungiwa Mwelusi, ni vikaragosi wa utawala kwani wanaomba usiku na mchana ili Bokono aendelee kuiongoza Butangi. Maombi haya yao yalitokana na maovu waliyoyatekeleza walipokuwa katika kikosi kingine cha askari. Haswa walikuwa wakiwatesa na kuwauwa washukiwa na kuwazika mwituni.

Atega anatangaza kwa ujasiri mkubwa kwamba, viongozi na vikaragosi hao wangeshtakiwa chini ya Baraza La Hukumu ambalo lingeundwa upya.

Katika *Seserumbe,* ukaragosi unajidhihirisha kupitia Yamwaka. Huyu ni tarishi na msiri wa Seserumbe. Anampigia debe waziri huku akijua kuwa ni kiongozi asiyewajibika. Anaahidi kuendelea kuuimba wimbo wake hadi pale uongozi wake utakapofika kikomo. Kulingana na Yamwaka, Seserumbe ni mbunge na waziri wa kudumu. Katika kampeni za ubunge Yamwaka anasema:

> ...Nami nataidi...Kupe hung'ang'ania kwenye ngozi ya ng'ombe hadi itakapoambwa ikauke...Uchaguzi ujao hali itakuwa kama kawaida, mzee ataibuka kama kiongozi kwa mara nyingine. Juhudi zozote za kumnyonyoa manyoya yake ya maendeleo na ufanisi zitagota ukuta wa ukweli. Ukweli ni kuwa Mzee ni mbunge na waziri wa kudumu! (uk 69).

Kembo anapouporomosha uongozi na uwaziri wa Seserumbe, huo unakuwa ndio mwisho wa Yamwaka na vibaraka wote wa Seserumbe.

**HITIMISHO**

Katika sura hii tumejadili dhana ya vijana na kulibainisha kundi la wanajamii tunaowaangazia katika kuleta mabadiliko. Tumeweza vilevile kuyajadili maovu ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Haya ni maovu ambayo vijana wameweza kuyatambua na kukabiliana nayo ili kuleta mabadiliko katika jamii zao kwenye tamthilia tunazozihakiki.

Maovu tuliyoweza kuyajadili ni pamoja na udikteta, ufisadi, dhuluma, unafiki na vita vya kikabila kutokana na uchochezi. Tumeweza kutoa mifano ya kutosha kuwaonyesha vijana wakizua upinzani dhidi ya viongozi waovu. Wakiwa kwenye mstari wa mbele vijana

wameonyeshwa wakipambana ili kuyaondolea mbali maovu haya na kuleta hali nafuu katika jamii zao. Kwa hivyo vijana wamejidhihirisha kama kundi linalofaa kutambuliwa kama washika dau wanaostahili kushirikishwa kwenye maamuzi katika mahusiano ya mamlaka

# SURA YA TATU

# MAFANIKIO NA CHANGAMOTO ZINAZOWAKABILI VIJANA KATIKA JITIHADA ZAO ZA KULETA MABADILIKO

## 3.0 UTANGULIZI

Katika sura hii tunaangazia mafanikio wanayoyaafikia vijana katika jitihada zao za kuleta mabadiliko katika jamii kulingana na tamthilia nne tulizoziteua. Tumeweza kuwaonyesha vijana kama watu wakakamavu, wenye nishati na wenye kujitolea katika mambo wanayoyaamini. Vilevile, tumejadili changamoto wanazokumbana nazo katika jitihada zao. Haya ni mambo yanayokwamisha au kutowezesha mabadiliko kamili kutokea kwa wakati ufaao.

Kwanza tumejadili namna vijana walivyofanikiwa kuleta mabadiliko chanya katika jamii zao. Hapo baadaye tunazijadili changamoto zinazowakabili katika jitihada za kuafikia kuleta mabadiliko katika tamthilia nne tunazozihakiki.

### 3.1.1 KUWAONDOA MADIKTETA UONGOZINI

Katika *Kifo Kisimani,* Bokono aliondolewa uongozini na wazalendo. Wakiongozwa na kijana jasiri, Atega, waliweza kuingia kwenye makao makuu na kuwaamrisha waliokuwepo kusalimu amri. Bokono na wenzake wanapofungwa mikononi, Atega anawaeleza Wanabutangi kuwa viongozi waliokuwa na makosa wangehukumiwa na Baraza la Hukumu. Baada ya kuwafunga Bokono, Batu Mweke na Gege mikono, Atega anamzuwia Askari I kuwaadhibu kwa shoka na badala yake anasema:

> La! Usimwage damu...waambie watu watulie. Watukufu watatolewa nje sasa hivi. Waeleze kwamba, jukumu la

> kutoa hukumu si letu. Kazi hiyo tutaliachia Baraza La Hukumu.(uk.104)

Batu anajaribu kuomba msamaha wakati wanamapinduzi wanapoingia katika ikulu. Hii inaonyesha kwamba hata yeye anaelewa kwamba alikuwa na makosa na ndiyo sababu anaingiwa na hofu ya adhabu ambayo ilimsubiri.

Hapa tunayaona mabadiliko makubwa kwani Atega anawazuia wazalendo wenzake wasifanye kitendo cha kikatili na badala yake wasubiri makosa ya viongozi waovu kuamuliwa kisheria.

Mabadiliko yalitokea Butangi kama tunavyodhihirishiwa na mmojawapo wa wazalendo:

> ...mkono mrefu ulikuwa unajaribu kuyashambulia mabadiliko, mabadiliko yakaukwaruza kidogo.(uk.103).

Hii inamaanisha kwamba, mabadiliko waliyokuwa wakiyapigania yalikuwa yameafikiwa. Kufanikiwa huku kunajidhihirisha pale tunapowaona watu wengi wakijiunga na wanamapinduzi. Kuna wale waliokuwa uongozini, ambao hawakufurahishwa na udikteta wa Bokono. Hao ni pamoja na Kame, moja wa washauri na Askari I ambaye daima aliwapinga wenzake walipofanya makosa.

Katika *Pango,* Katango amefaulisha kutiwa mbaroni kwa Ngwese. Anafanya hivyo kwa kuwaarifu watu wanaomfumania katika tendo la kuirina asali bila ruhusa ya Wachemwa. Ni wazi kuwa Ngwese alipatikana na makosa ya kufuja pesa za umma na pia kushirikiana na wakoloni kuipora asali ya Wachemwa.

Baada ya Ngwese kukamatwa ni bayana kuwa Katango ambaye alikuwa mpinzani wa pekee wa Ngwese, alipewa kazi ya kuwa mlinzi wa pango. Kazi hii alikuwa tayari kuifanya kwa njia ifaayo ili kuwafaidi raia wote kama anavyosema:

..Sasa macho tumeyafungua

Sasa upofu tumeupofua

Sasa vinywa tumevifungua

Maovu nayo tumeyafukua. (uk.88).

Mwishowe, watu wote wanakubali kuwa Katango ni mkweli na alistahili kuwa mlinzi wa pango. Wanasherehekea na kumbeba kuashiria kuwa, wamemwidhinisha kuwa kiongozi wao. Kwa hivyo, Katango anajitokeza kama kielelezo cha kijana aliyepigania mabadiliko na kuwa kiongozi katika jamii yake.

Katika *Seserumbe,* Kembo na Maribel wamefaulu kumtangua waziri Seserumbe toka uongozini. Kembo anamshinda Seserumbe katika uchaguzi wa ubunge katika eneo la Madongoporomoka. Baada ya kukosa kiti cha ubunge, Seserumbe anapoteza wadhifa wake kama waziri. Maribel anamfahamisha babake kuwa, lazima afikishwe mahakamani kwa vile serikali mpya ilipigania mabadiliko. Maribel anamweleza babake kuwa, hawezi kushiriki ufisadi wa kubatilisha sheria ili babake asishtakiwe kama anavyosema:

...Raia wenyewe walikubali kuwa hiki ni kipindi kingine!

Walisema lazima wakate kiungamwana kinachounganisha

na matendo ya jana.(uk.98).

Hatimaye, sauti kali inamsuta Seserumbe kwa kumkumbusha kuwa alikuwa amekataa kutambua mkondo wa mambo. Anakumbushwa kuhusu matukio ya Madongoporomoka. Anakumbushwa makosa yake ya kubatilisha orodha za waliotakiwa kuachishwa kazi na woga wake baada ya kushindwa katika uchaguzi. Hizi zote zilikuwa sababu zake za kuporomoka hadi kunyonyoa manyoya asiweze kuruka tena.

### 3.1.2 KUBADILI MAWAZO

Tamthilia ya *Maua Kwenye Jua la Asubuhi,* inaandama mabadiliko kwa mtazamo tofauti. Vijana katika jamii ya tamthilia hii wanayaangazia maovu ya chuki, uchochezi na vita vya kikabila. Kulingana nao mabadiliko yanayofaa kuwepo ni ya kimawazo. Hii ni kwa sababu makabila mawili ya Wandiku na Watange yaliamini kuwa uhasama wao unaweza kuoandolewa mbali kwa vita. Fikra za Watange zilikuwa kwamba Wandiku ni wezi waliotoka kwao Makuyuni kuja kuyavamia mashamba yao. Palikuwepo na uchochezi mkubwa baina ya watu wa makabila haya mawili uliopelekea uhasama baina yao. Ndiyo maana kila moja ya makabila haya yametokea kuwa na wafadhili wa vita.

Waito na Nali ni vijana wawili waliokuwa katika mstari wa mbele katika kuzibadilisha fikra za wazee wa makabila yao. Waito aliwakabili Kabitho na Tungai kwa upande wa Wandiku. Aliwaeleza kuwa, vita husababisha maafa na hasara kubwa. Badala ya vita anawapendekezea kuzitumia njia badalia za kutatua migogoro iliyokuwepo baina yao na Watange.

Nali ambaye ni Mtange anakabiliana na babake Chebwe. Huyu ndiye mbabe wa kivita aliyekuwa akiwafadhili Watange huku akiwa na ndoto ya kuchaguliwa kuwa waziri. Nali anamweleza babake kuwa hata Wandiku walikuwa na uwezo wa kununua zana za vita. Kwa hivyo, iwapo kila kabila lingenunuwa zana kali kuliko lenzake, basi pangetokea maafa makubwa. Anamwomba babake aelewe kuwa Wandiku wa kawaida hawakuyapora mashamba yao ila palikuwepo na wamiliki wachache wenye maelfu ya ekari. Kwa hivyo pendekezo lake lilikuwa sheria ifuuatwe ili tatizo la umiliki wa ardhi utatuliwe.

Hatimaye tunamwona Tungai akiwa amebadili mawazo yake na kukubaliana na vijana kuwa, njia ya maandamano ingeweza kutumika katika kuitatua migogoro iliyokuwepo. Anawaaambia vijana:

> ...Huenda maandamano yenu yakafungua watu macho na
> kugundua kwamba viongozi wanawatumia tu... (uk. 80).

Tungai pia anadokeza kuwa, Chebwe na wapiganaji wenzake, walikuwa wameonyesha nia ya kutafuta suluhu kwa mazungumzo badala ya vita. Tunauona huu kama ushindi mkubwa wa vijana katika kuyabadilisha mawazo na fikra za wazee katika jamii yao.

### 3.1.3 KUWATAFUTA VIONGOZI WAPYA

Katika *Pango*, Katango anapewa wadhifa wa kuwa mlinzi wa pango. Hii iltokea baada ya kufumaniwa kwa Ngwese na wenzake wakiirina asali pangoni. Anawaahidi raia wenzake kwamba, kwa vile walikuwa wameyashuhudia maovu ya Ngwese, sasa wangeendelea kwa uongozi bora.

Katika *Seserumbe,* Kembo anafaulu kuwa mbunge wa eneo la Madongoporomoka na vilevile kuwa waziri. Huu ulikuwa ushindi mkubwa kwa vijana ambao walipigania mabadiliko. Kulingana na Maribel, viongozi waliochukua uongozi, walikuwa na azma ya kuhakikisha haki inatendwa bila ufisadi wowote.

Katika *Kifo Kisimani,* Atega anajitokeza kama kiongozi wa kimapinduzi kwa jinsi ambavyo anatoa amri na watu kuzingatia. Huu ni wakati ambapo wanamapinduzi waliingia katika ikulu na kuwafunga kwa kamba Bokono na wenzake. Yeye ni kiongozi mpenda haki kwa vile anawaamuru wenzake wasitumie mabavu kuwaadhibu viongozi waliotolewa madarakani na

badala yake uamuzi wa Baraza la Hukumu usubiriwe. Ni bayana kuwa Atega angepewa nafasi kubwa ili kuhudumu katika serikali mpya. Hii ni kwa kutilia maanani kuwa yeye na marehemu Mwelusi walikuwa waasisi wa mapambano yenyewe.

Katika *Maua Kwenye Jua la Asubuhi,* Waito na Nali wamepanga kuwa viongozi katika maandamano ya kupinga vita vya kikabila. Hii ni nafasi muhimu huku ikichukuliwa kwamba, uhasama baina ya makabila yao ulikuwa umedumu kwa muda mrefu. Walikuwa ni waasisi wa harakati muhimu za kuleta mabadiliko bila umwagikaji wa damu.

### 3.1.4 KUFICHUA KASHFA ZA UFISADI

Katika tamthilia ya *Pango,* Katango anafaulu kumdhihirisha Ngwese kama kiongozi fisadi asiyefaa kupewa jukumu la kulinda raslimali za umma. Anauonyesha ubinafsi wake katika kushirikiana na walowezi katika kuifilisi pango.

Kilele cha mafanikio ya Katango ni pale anapowafumani Ngwese wakiwa tayari kuirina asali kiharamu. Hii ni kashfa kubwa kwani alikuwa akiiuza asali katika nchi za kimagharibi huku akiwanyima raia haki yao. Hii ikujumuishwa na ufisadi wake wa awali zinamfanya kupoteza mamlaka ya kuwa mlinzi wa pango.

Katika *Seserumbe,* Kembo anafaulu kuzifichua kashfa zilizomhusu waziri Seserumbe. Kashfa hizi zilihusu matumizi mabaya ya pesa za wizara, ulanguzi wa dawa za kulevya, kuwatia watoto katika ajira haramu na kubatilisha orodha za majina ya waliostahili kustaafishwa kwa lazima. Kilele cha ufanisi wa Kembo ni pale ambapo Seserumbe alipokea barua ya kushtakiwa ili kujibu mashtaka ya ufisadi alipokuwa waziri.

Katika *Kifo Kisimani,* Atega anadokeza kwamba, Baraza la hukumu lingeundwa upya ili kuwafungulia mashtaka watu wote walioshirikiana na Bokono katika utawala wake wa

kidikteta. Katika mashtaka hayo, tunatarajia kwamba kashfa za watu walioshiriki kuwanyanyasa Wanabutangi zingefichuliwa na haki kutekelezwa kwa mujibu wa sheria.

### 3.1.5 KUTENDA HAKI BILA MAPENDELEO

Vijana wamejitokeza kama watu wapenda haki bila kupendelea. Kwa njia hii, tunaweza kusema kwamba wanafanya hivi kudhihirisha kwamba, panafaa kuwepo na mabadiliko ya mitazamo ya kuwaadilisha wanajamii kuwaiga kama vielelzo vya jamii mpya.

Katika *Seserumbe,* tunamuona Maribel, bintiye Seserumbe akimwambia babake kuwa hangeutumia uhusiano wake wa karibu na Kembo kubatilisha haki. Kwa hakika waziri alitarajia kwamba, bintiye angemwonea imani baada ya kuletewa barua ya mashtaka.

Maribel alikuwa tayari kuwatetea wafanyikazi bila kuuingiza uhusiano wa kifamilia katika mahusiano kazini. Kulingana na Seserumbe, hilo halingewezekana na ndio sababu akamwachisha kazi kwa kuogopa kuwa bintiye angemsaliti kwa yale aliyoyajua kutoka nyumbani.

Katika *Pango,* Katango hakujali kuwa babake angeenda gerezani baada ya kufumaniwa akiwa kwenye genge la Ngwese walipokuwa wakipora pango. Hii inamfanya kuaminika kama mwanamapinduzi kamili kwani watu wangefikiria kuwa angemtetea babake.

Katika *Maua Kwenye jua la Asubuhi,* Waito na Nali wanakabiliana na mababe wafadhili wa vita bila kujali kama walihusiana nao kifamilia. Waito anawakuta Kabitho na Tungai na kuwaambia ukweli huku akijua kwamba Kabitho alikuwa mjombake naye Tungai alikuwa mumewe dadake Kabitho. Naye Nali anakabiliana na babake kwa ujasiri na kumweleza waziwazi kuhusu uhusika wake katika matayarisho ya vita.

Haya yote yanatuonyesha kuwa vijana wako tayari kuyabadilisha mawazo katika jamii ambayo huchukulia kwamba ni lazima mtu kuwapendelea watu wa jamii au kabila lake. Badala yake vijana wangependa kuona kuwa haki imetendeka bila kupendelea ili wanajamii wote waliokandamizwa wafaidike.

## 3.2 CHANGAMOTO ZINAZOWAKABILI VIJANA KATIKA JITIHADA ZAO ZA KULETA MABADILIKO

### 3.2.0 UTANGULIZI

Katika sehemu hii tunazichunguza changamoto zinazowakabili vijana katika jitihada zao za kuleta mabadiliko katika tamthilia nne tulizoziteua. Tunayajadili mambo mbalimbali yanayokwamisha mabadiliko ambayo vijana wangependa kuyaona yakitekelezwa katika jamii zao. Baadhi ya maswala tunayoyajadili katika sehemu kama vile kutotahadhari kwa vijana na ukosefu wa mipango mwafaka ya baadaye katika uongozi yanaweza kutajwa kama udhaifu wa wasanii. Hii inatokana na wazo kuwa iwapo wasanii hawa walitarajia kuwasawiri vijana kama mawakala wafanisi wa mabadiliko chanya, basi hawakuwapa makali ya kutosha ili kulifanikisha lengo hili.

Changamoto tulizozijadili ni pamoja na mitazamo hasi ya wanajamii kuhusu vijana, ushawishi unaoleta usaliti, kutotahadhari na ukosefu wa mipango mwafaka ya baadaye.

### 3.2.1 MITAZAMO HASI KUHUSU VIJANA

Kuna mitazamo hasi kuhusu uwezekano wa vijana kushikwa nafasi za uongozi katika jamii. Kutokana na mitazamo hii vijana wanadharauliwa na kukejeliwa na viongozi au wanajamii wenzao.

Katika *Seserumbe,* waziri anaonyesha kutokuwa na imani na vijana katika maswala mbalimbali. Kwa mfano anapomwambia Kembo aandike hundi, anamwita mwoga asiyejua jinsi ya kujinufaisha maishani. Pia katika kampeni za kiti cha ubunge, Seserumbe anawadhihaki vijana kwa kuwaonyesha kama wanagenzi wasioweza kuumudu uongozi. Anawaona vijana kama wanaorukiarukia mambo kama anavyosema:

> ...Uongozi si ule mchezo wa kijana aliyekwenda kuwafunga wanyama na kuanza kuchezea na watu kumhusu mbweha... (uk.88).

Hii inamwonyesha Seserumbe kama mtu aliye na mtazamo hasi kuhusu vijana kwani tunajuwa kuwa Kembo alikuwa anaweza kuimudu kazi yake hata kuliko vile yeye alikuwa.

Katika *Pango,* tunamuona Ngwese akiuendeleza mtazamo hasi dhidi ya vijana. Anadai kuwa Katango hawezi kuwa mlinzi wa pango kwa sababu yeye kama vijana wengine ana papara nyingi wala hazijui dhiki za wanajamii (uk.46). Vilevile anamwona kama asiyekuwa na busara inayostahiki kiongozi. Kulingana naye:

> ...uongozi ni busara sio ya kijana ambaye hata meno ya maziwa hayajamtoka!...viongozi wa kesho! (uk.41-42)

Katika *Kifo Kisimani,* Gege ana mtazamo hasi kuhusu juhudi za nduguye Mwelusi kushiriki kwenye siasa za kumpinga Bokono. Anamshauri Mwelusi aache shughuli za umma na badala

yake atafute mke mrembo aoe na kupata watoto wake mwenyewe. Hapa tunaona kuwa, ndugu hawa wawili walikuwa na falsafa na mitazamo kinzani katika maisha yao.

### 3.2.2 USHAWISHI WAVIONGOZI WALIO MADARAKANI.

Ushawishi ni hali ya mtu kumbadilisha mwenzake fikra ili atende mambo kulingana na mawazo yake au aghairi kutekeleza mambo iliyoyaazimia. Ushawisi huu unaweza kutekelezwa kwa njia mbalimbali zikiwemo; kurairai, kuhonga au hata kutishia.

Katika *Kifo Kisimani,* Mwelusi anakabiliwa na majaribu makubwa kutoka kwa washauri wa Bokono. Kwanza, Batu anatumia woga katika kumshinikiza Mwelusi kukiri uchochezi. Kisha anapoona kuwa hatetereki katika msimamo wake, anamwahidi utajiri wa ardhi, mifugo na uongozi wa vijana. Haya yote Batu anayafanya ili kumshawishi Mwelusi kutupilia mbali upinzani wake kwa utawala wa Bokono.

Ushawishi mwingine unawahusu makachero waliomhadaa Gege kumsaliti Mwelusi. Wanajaribu kumshawishi kwa kumwahidi ndoa na bintiye Bokono. Hapa waliujua udhaifu wa Gege na kwa hivyo, wanafaulu anapomuua Mwelusi. Ushawishi wa aina hii unatumika na utawala wa Bokono ili kuuondoa upinzani wa vijana.

Katika *Pango,* tunamuona Ngwese akitumia vishawishi vya machungwa hadharani wakati wa uchaguzi. Kwa kweli hii ilikuwa ni hongo iliyowashawishi wapiga kura kubadilisha msimamo wao. Wengi waliokuwa wanamuuga Katango mkono walibadili nia na kumpigia Ngwese kura. Vilevile baada ya Ngwese kushinda na kuwa mlinzi wa pango, anaonyesha nia ya kumhonga Katango ili abadilishe fikra na kuwa muungaji mkono wa uongozi wake kama anavyosema:

> …nitamgeuza mfuasi wangu…najua siri yake…Pesa bwana! Hiyo ndiyo dawa yake! Sawa na mimi na wewe…anayenipinga ninamlainisha kwa pesa.(uk.83).

Katika *Maua Kwenye Jua la Asubuhi,* vijana wanashawishiwa na viongozi wa kikabila kwa njia mbalimbali. Njia ua kwanza inayotumiwa na Chebwe ni kuwalisha vijana kiapo cha kuwaaminisha kuwa walikuwa wakipigana vita ili kujihami dhidi ya Wandiku. Njia ya pili ni kwa kutumia vitisho kama anavyomtolea Toiche alipotaka kuasi kambi ya wapiganaji wa Watange.

Kwa upande wa Wandiku, Kabitho alitumia vishawishi vya pesa ili kuwanasa vijana ili washiriki katika vita vya kikabila. Anatumia pesa ili kumshawishi Walila kuwakusanya vijana watakaopigana kwa niaba ya Wandiku kama anavyosema:

> …kumbuka, Walila, kwamba mbali na pesa nitakazokulipa, wewe ni Mndiku. Una wajibu wa kuwasaidia Wandiku kujitetea…(uk.44).

Vilevile kijana aliyeitwa Chugu anawaeleza Waito na Nali kuhusu ziara waliyoifanya pamoja na rafiki yake Chengi. Anasema walikuwa wameenda kujiunga na wapiganaji Wandiku kwa ahadi ya kulipwa na pesa zilizotolewa na Kabitho. Hii inaonyesha kuwa vishawishi vilitumiwa kwa vijana ili kuwafanya washiriki katika vita vya kikabila vilivyopangwa.

### 3.2.3 VIJANA KUTOCHUKUA TAHADHARI

Vijana wanaonekana kuwa watu wasiokuwa na tahadhari wanapojitosa katika harakati za kuleta mabadiliko. Hawaonekani kung'amua kwamba, hiki ni kinyang'anyiro cha mamlaka

chenye hatari. Ni wazi kuwa viongozi waliopo madarakani hawataki kuondoka na kwa hivyo, wanapotumia mikakati hatari ya kujidumisha uongozini tungewatazamia vijana kutahadhari ili wafaulishe jitihada zao.

Katika *Kifo Kisimani,* tunamwona Mwelusi kama aliyekosa tahadhari kwa jinsi alivyokabiliana na utawala wa Bokono. Alifaa kujihadhari na mbinu za Bokono na washauri wake. Pia anakosa tahadhari dhidi ya kakake Gege aliyemjua kama asiyependa harakati alizoziandama. Ilifaa Mwelusi kuwa na walinzi pamoja na washauri wake ili ayaendeleze mapambano hadi mwisho. Vilevile alipokabiliana ana kwa ana na Zigu, aliyahatarisha maisha yake kwani Zigu angemuua kwa urahisi akikitumia kisu alichokuwa nacho.

Katika *Maua Kwenye jua la Asubuhi,* tunawaona vijana wawili wanamapinduzi wakikabiliana na wafadhili wa vita vya kikabila bila tahadhari yoyote. Nali alifanya kitendo hatari cha kwenda kumtafuta Waito kwao huku akijua kuwa, anaingia katika eneo la maadui. Aliposhikwa mateka angeuwawa kwa urahisi isipokuwa Tungai alimkuta kisadfa na kumsaidia.

Katika *Pango,* Katango aliyahatarisha maisha yake alipokaribia pango na kuwashuhudia Ngwese na wenzake wakijitayarisha kuirina asali. Ni kwa kujihatarisha jinsi hii ndipo Ngwese aliweza kumtia kitata asiweze kuongea.

Hata hivyo tunaweza kusema kuwa vijana walikuwa watu jasiri ambao hawakuwaogopa viongozi na hili ndilo lililofanikisha mabadiliko tunayoyashuhudia katika tamthilia nne tulizoziteua.

### 3.2.4 UKOSEFU WA MIPANGO YA SIKU ZA BAADAYE.

Kwa kutokuwa na tajriba, vijana hawakuwazia hali ambayo ingefuatia baada yao kufaulu kuleta mabadiliko. Kwa hivyo, wanaishia kuondolea mbali uongozi katili bila mpango wa nani na vipi wangechukua hatamu za kuongoza. Kwa hivyo, mabadiliko yao yanaishia kusherehekewa kwa muda mfupi, kisha wazee wanakabidhiwa uongozi huo tena. Huu tunaweza kuuchukulia kama udhaifu wa wasanii ambao hawatupatii mwelekeo au mapendekezo ya viongozi waliotarajia kuiongoza jamii

Katika *Kifo Kisimani,* baada ya wanamapinduzi kujitoma na kuwaondoa Bokono na vibaraka wake, hapakuonekana pakiwa na mipango kamili kuhusu ni nani aliyetarajiwa kuwa kiongozi wa Butangi. Inajitokeza kuwa baada ya kifo cha Mwelusi, aliyechukua jukumu la kuwaongoza wazalendo alikuwa ni Atega, ila hakuna dalili zozote za kuonyesha kuwa angeteuliwa kuwa Mtemi. Ukosefu huu wa mipango ya baadaye ni mojawapo upungufu wa msanii kwa kukosa kutoa mapendekezo yake kuhusu nani au jinsi gani Butangi ingepata kiongozi mwajibikaji.

Katika *Maua Kwenye Jua la Asubuhi,* Waito na Nali hawakutufafanulia kuhusu jinsi wangeleta maridhiano miongoni mwa watu kutoka makabila ya Wandiku na Watange. Vilevile hatukuambiwa kuhusu mashamba yaliyokuwa yamechukuliwa na Watenge. Hii inatufanya kusema kuwa vijana walikuwa wazuri sana katika kuzianzisha harakati za mabadiliko na kuyafaulisha lakini wakakosa mipango ya utekelezaji wa baadaye.

### HITIMISHO

Katika sura hii tumejadili mafanikio na changamoto ambazo vijana wanakabiliana nazo katika harakati zao za kuleta mabadiliko chanya. Miongoni mwa mafanikio walioweza kuyaafikkia ni pamoja na kuwaondoa madikteta uiongozini, kuzifichua kashfa na kuzingatia utendaji haki bila kupendelea na kuzima mipango ya vita vya kikabila.

Changamoto tulizozijadili ni pamoja na mitazamo hasi, usaliti, ukosefu wa mipango ya baadaye na kutokuwa na tahadhari kwa vijana. Tumekwishataja kuwa ukosefu wa mipango ya baadaye na kutotahadhari kwa vijana zinaweza kuchukuliwa kama udhaifu wa wasanii ambao hawakuwapa vijana makali ya kutosha ili kuafikia ufanisi wa jitihada zao. Vilevile wasanii walikosa kutoa suluhu au mielekeo ya hatima ya mabadiliko.

# SURA YA NNE

# HITIMISHO

## 4.0 UTANGULIZI

Katika sura hii tumetoa muhtasari wa utafiti wetu. Tumedhibitisha namna vijana wanalivyojitokeza kama mawakala wa kuleta mabadiliko chanya katika jamii zilizosawiriwa katika tamthilia nne tulizoziteua. Aidha tumeeleza matokeo ya utafiti wetu kabla ya kuhitimisha kwa kutoa mapendekezo ya utafiti zaidi kuhusiana na mada yetu.

## 4.1 MUHTASARI WA UTAFITI

Utafiti huu umelenga kuchunguza vijana kama wahusika wenye uwezo wa kuleta mabadiliko kama walivyosawiriwa katika tamthilia nne za Kiswahili zilizoandikwa katika mwongo wa kwanza wa karne ya ishirini na moja. Tamthilia hizo ni *Kifo Kisimani (2001)* na *Maua Kwenye Jua la Asubuhi (2006)* zilizoandikwa na Kithaka wa Mberia. *Pango (2003),* na *Seserumbe (2009)* zilizoandikwa na K.W. Wamitila.

Katika tamthilia hizi nne motifu ya mabadiliko inayoendelezwa na juhudi za wahusika vijana imejitokeza. Vijana hawa wameweza kuyatambua maovu ya viongozi na kuwazindua wanajamii ili kuwaondoa viongozi hao madarakani. Viongozi walioondolewa madarakani ni pamoja na Mtemi Bokono katika *Kifo Kisimani*, Ngwese katika *Pango*, na waziri Seserumbe katika *Seserumbe.* Vijana vilevile wameweza kuondolea mbali matayarisho ya vita vya kikabila katika *Maua Kwenye Jua la Asubuhi.*

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Ki-Foucault ambayo mwanzilishi wake ni Micheal Foucault. Nadharia hii hupendekeza kuwa katika jamii, huwa kuna mahusiano ya mamlaka ambayo huhusishwa na mikakati ya kutawala na kutawaliwa. Mahusiano haya huzalisha upinzani pale panapozuka ukiukaji wa maadili. Wanajamii hupambana ili kujirejeshea uwezo wa kuyarahisisha maisha yao dhidi ya mifumo dhulumati.

Ni upinzani huu tulioufuatilia katika tamthilia hasa unaoongozwa na vijana wanaojitahidi kubadilisha maisha ya watu walionyanyaswa. Katika *Kifo Kisimani,* Mwelusi na Atega ni vijana wanaoupinga udikteta wa Mtemi Bokono na kuwahimiza Wanabutangi kuipindua serikali ya Bokono. Katika *Pango,* uongozi wa Ngwese unapingwa vikali na vijana kama Katango na Kibwana. Hawa wanahakikisha kuwa wameufichua ufisadi wa Ngwese hadi pale anapotiwa mbaroni kwa mashtaka ya kutumia mali ya umma vibaya. Katika *Seserumbe,* waziri Seserumbe anapingwa vikali na kijana Kembo kutokana na utumizi mbaya wa pesa katika wizara pamoja na matendo mengine yasiyozingatia maadili. Hatimaye, kijana huyu anamshinda Seserumbe katika uchaguzi wa eneobunge la Madongoporomoka. Waziri huyo anashtakiwa kwa makosa ya kutumia pesa vibaya katika wizara

Vilevile wanajamii kaitika maingiliano yao kulingana na nadharia ya Ki-Foucault, huongozwa na mawazo ambayo yanaweza hubadilishwa ili kuzua hali nafuu za kiuhusiano. Ni mawazo kama hayo yanayoangaziwa katika *Maua Kwenye Jua la Asubuhi.* Hii ni jamii yenye makabila mawili yanayozozana kutokana na fikra kuwa kabila la Wandiku, limeipora ardhi ya Watange. Na kwa hivyo, Chebwe anawafadhili wapiganaji ili kuwafukuza Wandiku kutoka mashambani mwao. Kabitho naye anawafadili wapiganaji wa Kindiku ili kupigana na Watange. Kulingana naye hii ingewawezesha kuyahifadhi mashamba waliyokuwa wameyanunua. Vijana katika tamthilia hiyo wanafaulu kuzibadilisha fikra na mawazo ya wazee wao kwa kuwahimiza kutumia njia badalia za kusuluhisha migogoro baina yao.

Katika sura ya kwanza, tumechunguza maswala ya kimsingi yanayodhamiria kujengea msingi wa utafiti wetu kama sababu za kushughulikia mada, tatizo la utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, upeo na mipaka ya utafiti. Tumeongozwa na nadharia tete zifuatazo: kwamba vijana wamefanikiwa kuyaleta mabadiliko katika tamthilia nne na kwamba wanakabiliwa na changamoto mbalimbali katika jitihada zao.

Katika sura ya pili, tumeyachunguza maovu ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Tumeweza kuwaonyesha vijana wakikabiliana na maovu hayo. Tumeweza kuujadili udikteta na mikakati ya viongozi wa kiimla na kuonyesha jitihada za vijana wakiwaongoza wanajamii ili kuwaondoa mamlakani. Madikteta kama vile Bokono katika *Kifo Kisimani,* Ngwese katika *Pango na* waziri Seserumbe katika *Seserumbe* wameweza kuondolewa madarakani. Wote walipoondolewa walipangiwa kujibu mashtaka ya ufisadi na utumizi mbaya wa mamlaka.

Katika *Maua Kwenye Jua la Asubuhi,* vijana Waito na Nali wameweza kuwabadilisha mawazo wazee wao ambao ni wafadhili wa vita. Kabitho na Tungai wameamua kuwaunga vijana mkono katika kutumia maandamano kama njia ya kusuluhisha migogoro baina ya makabila ya Wandiku na Watange. Chebwe naye amekubali kutafuta uwiano kwa njia ya amani badala ya vita.

Katika sura ya tatu tumechunguza mafanikio waliyoyapata vijana katika kuzibadilisha jamii zao. Katika *Kifo Kisimani, Pango na Seserumbe,* kwa juhudi za vijana viongozi wa kimabavu wameondolewa madarakani. Vijana hawa ni pamoja na Mwelusi, Atega, Katango, Kibwana Kembo na Maribel. Viongozi makatili waliondolewa mamlakani ni Bokono, Ngwese na Seserumbe, hawa wangefikishwa mahakamani ili kushtakiwa kwa maovu waliyoyatenda. Vijana hawa tunawaona wakiwa wapenda haki kwa vile hawakuunga mkono utumizi wa fujo wala ukatili katika kuwahukumu viongozi hao.

Katika *Maua Kwenye Jua la Asubuhi,* vijana Waito na Nali wamefaulu kuleta mabadiliko ya kimawazo pale ambapo wanawazindua wazee wao kutokana na fikra kwamba, migogoro baina ya makabila ya Wandiku na Watange ingesuluhishwa kwa kutumia vita. Vijana hawa wawili wanawahimiza wafadhili wa vita kutoka pande zote mbili kubadilisha mbinu na kutumia maandamano ya kuvipinga vita. Hali kadhalika, wanautumia uchumba na ndoa kama njia ya kuyaunganisha makabila hayo mawili.

Katika sura hiyo ya tatu tumechunguza changamoto zilizowakabili vijana katika harakati zao za kuleta mabadiliko. Changamoto tulizoziangazia ni pamoja na mitazamo hasi, usaliti kutokana na vishawishi, kutotahadhari na kutokuwepo kwa mipango ya baada ya kuwaondoa viongozi hao waovu.

## 4.2 MATOKEO YA UTAFITI

Utafiti huu umehusu vijana wanavyochangia mabadiliko katika tamthilia nne za Kiswahili zilizochapishwa katika mwongo wa kwanza wa karne ya ishirini na moja. Tumeweza kudhibitisha kwamba:

- Vijana wanayatambua maovu ya kisiasa, kiuchumi na kijamii na kukabiliana nayo;
- Wamefanikiwa kuwaondoa viongozi waovu kutoka madarakani;
- Wanakabiliwa na changamoto katika harakati za kuleta mabadiliko;
- Nadharia ya Ki-Foucault kuhusiana na swala la uhusiano wa mamlaka limejitosheleza kuzihakiki tamthilia za *Kifo Kisimani, Pango, Maua Kwenye Jua la Asubuhi* na *Seserumbe.*

## 4.3 MAPENDEKEZO

Utafiti huu umechunguza vijana kama waleta mabadiliko katika tamthilia nne zilizoandikwa katika mwongo wa kwanza wa karne ya ishirini na moja. Tumetumia nadharia ya Ki-Foucault ambayo tuliamini imeafiki malengo yetu. Hata hivyo, swala la vijana na uhusika wao katika tamthilia lina mitazamo mingi kulingana na waandishi walivyowasawiri. Tungependa kutoa rai kwa watafiti wengine kuchunguza ukweli kwenye tamthilia za Kikenya au kulinganisha ufanisii wa vijana kuleta mabadiliko katika tamthilia na jamii halisi ya Kikenya.

Utafiti zaidi unaweza kufanywa kwa kuangalia mwingiliano wa fani na maudhui katika tamthilia hizo nne.

**MAREJELEO**


Arege, Timothy ( 2007 ) *Chamchela.* Nairobi : Jomo Kenyatta Foundation.

Becker, Eva (2011) Youth Rights in The Kenyan Constitution. Tasnifu ya uzamili ya chuo kikuu cha Uppsala. Sweden. (Ambayo haijachapishwa)

Brown, B.B. , Larson, R.W., Saraswathi, T.S.( Eds.) *(2002) The World's Youth: Adolescence in Eight Regions of the Globe*: United Kingdom. Cambridge University Press

Dorsch, T.S. (1965) *Classical Literary Theory* : Harmondsworth: Penguin.

Dreyfus, H. L. & Ribinow, P. (1982) *Micheal Foucault: Beyond structurarism & Hermeneutcs.* Chicago: University of Chicago.

Erikson, H. E(ed.) (1961) *Youth Change and Challange.* New York: America Academy of Art and Science.

Fisk, J. (1993), *Power and Power Works.* London: Verso Publishers.

Foucault, Micheal (1982) The subject and Power[Afterword] in Dreyfus H.L & Rabainow P. *Micheal Foucault: Beyond Structuralism and Hermeneutics.* Chicago. University of Chicago.

Foucault, Micheal (2000), *The Political Technology of Individuals.* New York: The New Press.

Hussein, E. N. (1971) *Wakati Ukuta.* Nairobi: East African Publishing House.

Hyslop, G. (1975) *Kulipa ni Matanga.* Nairobi: Nelson.

Kirkpatrick, Jean J. (1982). *Double Standards of Dictatorship.* New York: American Enterprice Institute.

Kitsao, Jay (1980) *Tazama Mbele.* Nairobi: Heinemann.

_________ ( 1980 b) *Uasi.* Nairobi: Oxford University Press.

Kuria, H. (1957) *Nakupenda Lakini...* Dar es Salaam: East African Literature Bureau.

Lwanga, E. (2007) *Youth Situation in Kenya.* Nairobi: United Nation Development Programme.

Mamuya, S.J. (1974) *Ujana.* Nairobi: Kenya Ritho Ltd.

Mazrui, A. na Njogu, K. (2006) *Sudana.* Nairobi: Longhorn Publishers

Mbatiah, M. (2006) *Migogoro.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Mberia, Kithaka ( 1997) *Natala.* Nairobi: Marimba Publishers.

________________( 2001) *Kifo Kisimani.* Nairobi: Marimba Publishers.

________________(2004) *Maua Kwenye Jua la Asubuhi.* Nairobi: Marimba Publishers.

Mlama, P. (1972) *Hatia.* Nairobi: East African Publishing House.

Mogambi, P.J.(1982) Uhakiki wa Maudhui Katika Tamthilia za Kiswahili za Kikenya Zilizochapishwa: tasnifu ya shahada ya uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi. (ambayo haijachapishwa)

Mohamed, S.A. (2000) *Kitumbua Kimeingia Mchanga.* Nairobi: Oxford Universty press.

_____________ ( 2011) *Janga la Werevu.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Mungai, J. na Uhinga, G.M. (1975) '*Nakupenda Lakini*,' katika Topan Farouk (mhr) (1975). *Uchambuzi Wa Maadishi Ya Kiswahili: Nairobi Oxford University Press.*

Mutonya, Mungai (2007) *Mnada wa Sokomoko*: Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Mutua, J. M. (2010) Mtazamo wa Vijana na Wazee Kuhusu Ukombozi wa Mwanamke Katika Tamthilia tatu za Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili. Chuo kikuu cha Nairobi.( ambayo haijachapishwa)

Ngugi, G. (1961) *Nimelogwa Nisiwe na Mpenzi.* Nairobi: EAPH.

Njonjo, S. Katindi, (2010) *Youth fact Book; Infinite Possibility or Definite Disaster?* Nairobi: Institute of Economic Affairs

Republic of Kenya (2010) *The New Constitution of Kenya.* Nairobi: Attoney General's Office.

Sercombe, H. (1997) *Power, Ethics and Youth Work.* Brandford: Edith Conwan University.

Scott, Grand (1999) *The Power of Youth*: www,http//mht

Topan, F. (1975) *Uchambuzi wa Maandishi Ya Kiswahili: Kitabu cha Pili.* Oxford: Oxford University Press.

TUKI. (1981) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Nairobi: Oxford University Press.

Wafula, R.M. (1999) *Uhakiki Wa Fasihi: Historia na Maendeleo Yake.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K.W. ( 2003) *Pango.* Nairobi: Focus Publishers.

____________( 2006e) *Sumu Ya Bafe*. Nairobi: Focus Publishers

____________( 2009) *Seserumbe.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

_____________ (2002) *Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: Phoenix Publishers.

_____________ (2008) *Kanzi ya Fasihi 1: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

Wellek & Warren (1949) *Theory of Literature.* Harmondsworth: Penguin.

Wikipedia (2012) *Micheal Foucault- Wikipedia the free encyclopedia.*